# Vitambulisho Vitano Thabiti Vya Kanisa La Kweli La Mungu Aliye Hai

Jeffersonville, Indiana, Amerika
Septemba 11, 1960

1 Asante, Ndugu Neville, Bwana akubariki. Hakika ni heshima kuwa hapa usiku huu. Nina furaha mno kwamba Mungu alituruhusu kufanya hilo. Ninaonea kamera haya kidogo. Napenda ... Endelea, zipige. Hilo ni sawa. Nazitazama tu. Nazitambua hizo. Na hilo ni sawa. Ni sawa. Sasa, ni joto kidogo. Tumekuwa na jumbe mbili nzuri sana kutoka kwa Bwana.

2 Na sasa nilifikiri, usiku huu, kwa kuona hilo ...

2

Wengi wa marafiki zangu wako hapa ambao inawapasa kuendesha magari umbali mrefu, baadhi yao kutoka chini kule Kentucky. Namwona Ndugu WElch Evans na familia yake hapa kutoka Tifton, Georgia. Nilikutana na watu nje hapa kutoka California. Kuna baadhi hapa kutoka Ujerumani na sehemu mbalimbali, wakija kwenye hii sehemu ndogo, ili kumtumikia Bwana. Na namwona Dada Nellie Cox. Naamini kwamba mama mkwe wake na wengine wako hapa. Ambapo, labda watarudi maili nyingi usiku huu katika Kentucky, Georgia, chini katika Tennessee, hadi Ohio, marafiki zangu hapa. Rafiki mmoja hapa, Ndugu Ted Dudley, kote kutoka Phoenix, Arizona. Kuna wengi wao hapa, wengine, kama ningewaita tu wao kwa majina, waliokuja hapa kututembelea leo. Asilimia tisini ya wao hata sijawagusa mikono yao. Nawaona rafiki zangu kutoka Chicago, na kote tu. Ni watu wangapi walioko ndani hapa kutoka nje ya mji, inueni mikono yenu. Asilimia tisini ya kusanyiko, sasa, hilo limefanya marafiki mbalimbali kutoka makanisa mbalimbali kote nchini.

3 3

Na nilihubiri kwa muda mrefu asubuhi hii, kuombea wagonjwa hadi saa saba na nusu, hivyo koo langu lilikwaruza kidogo. Na imenipasa kuhubiri kidogo kwa namna ya kuingia, kile tunachokiita, gia ya pili, kabla.

4

Yule pale Ndugu Lee Vayle. Sijawa na lingine na yeye zaidi ya kushika mikono yake, mmoja wa wasaidizi wangu; kanisa la Baptisti, Ohio.

5

Je, ni wewe, Ben? [Ndugu Ben Bryant anasema, "Amina."-Mh.] Sikuwa nimekusikia ukisema, "amina" bado, laa sivyo ningekuwa nimekujua. Wote mnamfahamu Ndugu Ben. Na najua yeye anatoka nje ya mji, hivyo sijui tu ... Unatokea wapi sasa, Ndugu Ben? [Vema, tuko North Borden, Indiana, ndugu."] Borden, Indiana.

4 6

Tuna furaha kuwa na kila mmoja hapa. Na sasa sitawaweka kwa muda mrefu, kwa sababu ya maili nyingi ambazo itabidi muendeshe magari. Natamani ningeweza kumchukua kila mmoja wenu nyumbani usiku huu. Kwa kweli namaanisha hilo. Inanipasa niondoke takriban saa tisa, kati ya saa tisa na saa kumi alfajiri, na na-natamani ningewachukua twende pamoja. Namwona rafiki yangu hapa kutoka Arkansas, mke wake. Je, wewe siyo yule mtu tuliyekuwa ... Bwana alinena naye na kusema haya mambo ndani hapa usiku ule mwingine? Na nilidhani ilikuwa wewe. Ninapotazama tu kote, unaona marafiki wapya na wa zamani. Hivyo, Mungu anajua makusudio ya moyo wangu, kwamba ningependa kupata kuwaona, na kuwapeleka nyumbani pamoja na mimi na kuwa na maongezi mazuri. Lakini siku moja tutafanya hilo. Pale ambapo hatutakuwa na kusema, "Inatupasa kuharakisha. Kwenda kuwachukua watoto. Mtu fulani ni mgonjwa." Yote hayo yatakuwa yamekwisha wakati huo, Siku ile kuu. Natumaini tutakutana mara nyingi zaidi.

5 7

Sasa, ni kusudio langu, ninapomsubiri Bwana sasa, ili kupata mwelekeo. Sasa, Jumanne, nakwenda kuhitaji maombi vibaya zaidi kuliko nilivyowahi kuhitaji hilo katika maisha yangu yote. Nakwenda kuwaomba kama mtaniombea. [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Ni-nitahitaji maombi yenu. Hakikisheni mnaniombea. Jinsi upepo unavyogeuka, Jumanne, huenda ikamaanisha jambo kuu kwangu, na kwa Kanisa na kwa ajili ya Kristo. Hivyo hakikisheni mnaniombea.

6 8

Sasa, basi, hadi nipate ni mwelekeo gani niende na nini cha kufanya, namsubiri Bwana. Wakati huo, nitakuwa kwenye hekalu hapa kuingia na kutoka, nikihubiri, kuombea wagonjwa, nikifanya chochote ambacho ninaweza kufanya. Tunataka, siku fulani, kama serikali haitatuzuia, tunataka kujenga kanisa hapa, kanisa zuri ambapo tunaweza na nafasi ya kutosha kuketi watu, sehemu kuu ya ukumbi, na kibaraza cha ghorofa, na kadhalika, hivyo litakuwa kanisa zuri hasa, lenye vibadilisha hali ya hewa, ili watu waweze kuketi kwa utulivu, wasikilize ibada, kama wataturuhusu tufanye hivyo. Sasa, tuombeeni.

7 Na sasa, usiku huu, tunakwenda kuliendea lile somo nililoliahidi, asubuhi hii, Bwana akipenda, kulizungumzia, usiku huu. Na inakwenda kuwa, zaidi, kufundisha, kwa sababu ya sauti. Nataka kunena, usiku huu, juu ya : Vitambulisho Vitano Thabiti Vya Kanisa La Kweli La Mungu Aliye Hai. Vithibitisho vitano thabiti vya Kanisa la kweli, au vitambulisho, kabisa, vya Kanisa la kweli!

8 10

Sasa, kabla hatujaliendea hili somo kuu na lenye nguvu, ninakwenda kuwatakeni neno la maombi. Nakwenda kumwomba mchungaji wetu, Ndugu Neville, kama yeye angekuja juu na kutoa maombi juu ya Neno la Mungu. Tunapofungua, sote, Mathayo Mtakatifu, ile sura ya 16, aya ya 18, kwa kuanzia, Mtakatifu Mathayo 16:18, wakati Ndugu Neville akija kwa ajili ya maombi ya faraja.

[Ndugu Orman Neville anaomba maombi yafuatayo-Mh.]

["Baba yetu wa Mbinguni, tunazo shukrani usiku huu kwa ajili ya hili, heshima nyingine na nafasi uliotupa, kupitia rehema Zako kuu, zisizokuwa na mwisho. Tunazo shukurani usiku huu kwa ajili ya mvuto na msukumo, na uongozi wa Roho Mtakatifu. Tunashukuru, Mungu wetu, kwamba Wewe ni Mungu uliyeshuka chini kuwa ndani yetu na kuwa pamoja na sisi, hadi mwisho wa ulimwengu huu."] Ndiyo.

["Baba, matatizo makuu na majaribu ya kesho hayatakuwa chochote maadam tunaweza kushikilia mkono Wako na kutembea kote pamoja na Wewe." Kwa kweli, Bwana. ["Tunaomba, Bwana, kwamba Wewe utatupa wema wa kilindi, mmoja kwa mwingine, tukijua kwamba mmoja anapokuwa katika kilindi cha jaribu, na ugumu wa kujaribiwa, kwamba sisi, pia, mojawapo ya siku hizi, tutapitia hali hizo. Mungu, utupe Roho wa Yesu ndani yetu, hadi kila mmoja ajisikie juu ya mwingine, vya kutosha, hadi kuwepo na muungano kati yetu, hadi tuweze kukutumikia Wewe, kwa pamoja."] Ndiyo.

["Baba, tunakushukuru, usiku huu, kwa ajili ya hii, heshima nyingine uliyotujalia, kuweza kuketi chini ya fundisho la mtumishi Wako ambaye Wewe ulimwekea tangu asili, ambaye Wewe ulimteua kuwa katika nafasi hii."] Asante. ["Ambaye Wewe uliona inafaa kuturuhusu sisi kuwa na heshima ya kuwa ndani, chini ya mafao ya hii huduma. Mbariki yeye na sisi, sote, kwa ... pamoja na hii huduma yeye aliyo nayo juu yake."] Tujalie hilo. Ndiyo.

["Baba, tunaomba kwamba wakati hizi siku zinapokaribia katika wiki inayokuja, wakati tutakapokuita Wewe sasa katika hii hali ya kuombewa, tukisema ndani ya mioyo yetu, kwamba, "Mungu, kwa kuwa ulituambia kwamba mambo yoyote tutakayoyasema, itakuwa kama tulivyolisema hilo, kama tutaamini na kutumaini na kukutii Wewe.' Kwa hiyo, Bwana, hizi siku zinazokuja ambazo zitakuwa jaribu juu ya ndugu yangu, na ndugu yetu, na mtumishi Wako. Ewe Mungu, tunamkabidhi Kwako, mno, katika Jina la Bwana Yesu, na kuomba kwamba utamzingira kwa ulinzi wa Kimbinguni na baraka ambazo hajawahi kuzijua hapo kabla."] Tujalie hilo, Bwana. Fanya, Bwana.

["Mungu wangu, tunaomba kwamba Wewe utaikandamiza kila nguvu ya kiakili itakayoinuka, ili kujaribu kushawishi kinyume au kujaribu kuweka kando."] Tujalie hilo, Bwana. ["Hebu mdomo wake ufunguke kwa maneno ya hekima kunapokuwa na nafasi yoyote ya kunena."] Ndiyo, Bwana. ["Ewe Bwana, tunakushukuru, Mungu wetu, kwamba

Wewe umefanya njia kwa ajili ya watumishi Wako wote, kote kwenye vipindi."] Ndiyo. ["Na Roho Mtakatifu amekuwepo kwa wingi kutoa maneno ya mdomo kwamba angesimama uweponi mwa watu wasomi na wenye akili."] Ndiyo, Bwana.

["Tunakuomba, Baba yetu, uturuhusu tutembee kwa unyenyekevu na upole, na mbele Yako, Ewe Bwana Yesu. Turuhusu tu kufanya mapenzi Yako na kuusikia Uwepo Wako. Uwe pamoja na sisi sasa. Na, Ewe Mungu, tunaomba kwamba sifa Yako kamilifu iwe ndani yetu, hadi ijitokeze, siyo ya nguvu, lakini sifa itatoka kwetu, pamoja na upako."] Ewe Mungu!

["Ee, Bwana wangu, usiku huu, maliza hii siku nzuri ambayo Wewe umekuja na kuponya wagonjwa, na umekomboa waliopotea, na umekuwa pamoja na sisi, ili kuitakasa mioyo ya walio wachafu."] Ndiyo! ...?... ["Sasa, Bwana, chukua mamlaka usiku huu, katika hii ibada, na ubariki koo la ndugu yetu. Na ubariki Neno linapotiririka. Hebu na tuwe na mioyo na akili za kupokea. Na, Ewe Mungu, sasa pokea sifa zetu kwa ajili ya hilo, katika Jina la Yesu. Amina na Amina."] Amina.

11

Je, hiyo ina sauti yote? Utaondoa ya kwako kwenye ...?... Ni yote? [Mtu fulani anasema, "Ni sawa."-Mh.] Je, hiki ni kipaza sauti, kipaza sauti chenyewe? ["Vyote viwili."] Je, mnaweza kuniskia vizuri? Kule nyuma, mnaweza kunisikia? ["Amina."] Sawa. Vema.

9 12

Natamani kusoma sasa kutoka kwenye Kitabu cha Mathayo, sura ya 16 na ile aya ya 18. Nitaanza na aya ya 17.

Yesu akajibu, akamwambia, Heri wewe Simoni Bar-yona; ... kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni.

... Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.

10 13

Mungu aongeze baraka kwenye Neno Lake. Neno Kanisa, juu ya kila moja ya haya masomo niliyoyachagua usiku huu, ili kujaribu kunena kwenu juu yake, mojawapo ni: Kanisa ni nini? Ni nani aliyeliweka Hilo? Ujumbe Wake ni nini? Jinsi gani tunakuwa washirika wa Hilo? Na je tunaweza kufika Mbinguni bila kuwa mshirika wa Hilo?

Sasa, kila moja ya hayo masomo, tungechukua saa kadha juu yake, tukipekua kwa makini mbele na nyuma. Lakini nataka tu kugonga mambo machache ya msingi ili kuonyesha kile Kanisa halisi lilicho. Na sasa nawataka ninyi mwe na Biblia zenu.

11 14

Sasa, jambo la kwanza, neno Kanisa, Lenyewe, humaanisha, "Walioitwa." Sasa, Israeli hawakuwa kanisa la Mungu maadamu walikuwa katika Misri. Wao walikuwa watu wa Mungu. Na ndipo Mungu alipowaita watoke Misri, wakafanyika kuwa kanisa la Mungu, kwa sababu wao walikuwa "walioitwa."

Sasa, hilo bado linabakia hivyo hivyo leo. Neno Kanisa humaanisha, "Wale walioitwa," wale waliokuwa wameitwa, waliotengwa, wakafanyika kuwa tofauti.

12 15

Sasa, katika Agano la Kale, Kanisa lililojulikana liliitwa 'Ufalme wa Mungu,‟ Ufalme wa Mungu. Sasa, nachukua hili kutoka katika wendo wa mfuatano wa matukio na majira ya Biblia. Agano la Kale, Kanisa liliitwa ″Ufalme wa Mungu.‟ Kwa maneno mengine, Mungu ni Mfalme na Kanisa ni milki Yake. ″Ufalme wa Mungu,‟ Agano la Kale.

16

Katika Agano Jipya, Hilo linaitwa "Himaya ya Kimasihi." Ee, nalipenda hilo, la Kimasihi. Katika namna nyingine, "Himaya ya Masihi," ambapo Masihi anamiliki na kutawala. Hakuna vizuizi vya kidhehebu au chochote, Masihi anatawala katika Ufalme Wake. Je, huko siyo kuwaza vizuri? Ufalme wa Kimasihi. Kwa hiyo, Kanisa siyo shirika, Kanisa siyo mkusanyiko wa watu. Kanisa ni watu wa Mungu ambao wameitwa watoke ulimwenguni, ili kutumika katika Ufalme mwingine.

13 17

Hili lingedumu kunukuliwa. Miezi michache iliyopita, mke na mimi tulikuwa tunakwenda sokoni. Na tukakuta kitu cha kigeni, kulikuweko na mwanamke barabarani, aliyekuwa amevaa sketi. Ah, usingeliweza kuamini hilo, lakini kwa kweli tulimkuta mmoja. Na mke akaniambia, "Vema, mtazame yule."

Nikasema, "Ni lazima yeye ni Mkristo. Yeye ni tofauti mno." Ni aibu.

19

Ndipo swali likaibuka, "Kwa nini iko hivyo, Bill, kwamba sisi, kama Wakristo, na hii Imani tunayoiamini, kwa nini tunawashurutisha wanawake wetu wavae magauni, ili kutenda namna ile? Watu wa makanisa mengine hawafanyi hivyo? Wao huvaa zile nguo namna hiyo, nguo za maadili mabaya, na ni kwa nini iko hivyo? Usingeweza kusema wao walikuwa na maadili mabaya."

20

Nikasema, "Hiyo ni kweli. Siwezi kumhukumu yeyote. Lakini, kwa kuwaona wao, 'Kwa matunda yao mtawatambua.' Huenda wao wasitende kosa, lakini juu yao kuna roho inayowaendesha kwenda kwenye maadili mabaya."

14 21

Sasa, Yesu alisema, "Yeyote amtazamaye mwanamke na kumtamani, amezini naye tayari katika moyo wake." Sasa, wakati yule mwenye dhambi atakapowajibika kwa kufanya uzinzi, ni yupi atakayekuwa mwenye hatia? Yule mwanamke aliyejipeleka mwenyewe. Huenda wewe ukawa msafi kama ua la yungiyungi, kadiri ya uadilifu ulivyo. Lakini kama umejiweka mwenyewe mbele ya watu, katika hali ya kiasherati, ingawa huna hatia ya tendo, ulimsababisha yule mwanamume kuwaza uovu juu yako, wakati ni kosa lako. Yesu alisema utakuwa na hatia ya "kufanya uzinzi." Na, "Mwanamke mzinzi kamwe hataingia Mbinguni."

15 Lakini, ninaposafiri ulimwenguni, nakuta kila taifa lina roho yake lenyewe. Na mataifa yote yanadhibitiwa na Shetani. Serikali zote zinatawaliwa na Shetani. Biblia ilisema hivyo. Hizo hupigana, hufanya vita, na zitafanya hivyo hadi Yesu ajapo, na ndipo Yeye ataweka Ufalme ambao hapatakuwepo na vita. Lakini Shetani alisema falme zote za ulimwengu zilikuwa zake, na yeye angelifanya nazo chochote yeye alichotaka, alisema moja kwa moja mbele ya Yesu Kristo. Na hizo zote ni vyombo vya Shetani, falme za Shetani. Shetani alimwambia Yesu, "Nitakupa Wewe hizo kama utaanguka chini na kunisujudia."

23

Yesu alijua angekuwa mrithi wa hizo, katika Utawala wa Miaka Elfu, hivyo Yeye akasema, "Ondoka hap, Shetani." Yeye alijua kwamba Mungu angelimpa Yeye falme zote, na zingekuwa za Kwake, na zote zingekuwa Ufame mmoja.

16 24

Unapokwenda Ujerumani, unakuta roho ya Kijerumani. Unakwenda Uingereza, unakuta roho ya Kiingereza. Unakwenda Sweden, unakuta roho ya Kisweden. Unakwenda Ufaransa, unakuta roho ya Kifaransa. Unakuja Amerika, unakuta roho ya Kiamerika.

Nilipita kule San Angelo, kule Rumi, kitambo fulani kilichopita, na nikataka kuona msururu wa makaburi chini ya ardhi. Na kwa mshangao, na kwa aibu, kwangu kama Mwamerika, nikiwa nimesimama mbele ya lango la msururu wa makaburi chini ya ardhi unapoingilia, linasema, "Kwa wanawake wa Kiamerika: tafadhali mvae nguo na kuwaheshimu wafu kabla ya kuingia hapa." Wakati Taifa linapozama chini kiasi hicho, inatisha, tunapofikia mahali hapo. Hivyo unaona, kwa sababu ...

17 Nilimwuliza mwanamke fulani wakati mmoja, "Je, wewe ni Mkristo?"

26

Akasema, "Mimi ni Mwamerika. Bila shaka, mimi ni Mkristo." Hilo halihusiani kwa chochote na hili.

27

Ndugu Bosworth alimwuliza mmoja, usiku mmoja, akasema, "Je, wewe ni Mkristo, dada?"

28

Akasema, “Nitakufahamisha, nawasha mshumaa kila usiku.” Kama vile hilo linahusiana na Ukristo, kuwasha mshumaa. Ukristo hauna vitu kama hivyo. Na Kanisa la Mungu halina mapambo kama hayo.

18 29

Sasa, kitu gani kinawafanya wanawake ... Kamwe hatujawalazimisha wanawake kufanya hilo. Hatukuwahi kuwalazimisha wanaume wetu kutokunywa pombe, wala kuapa. Tunahubiri tu Injili, na kuwawekea utaratibu wa Biblia. Wanaume wengi wanaokuja kwenye imani za Kipentekoste na imani za utakatifu, huingia ndani na kukiri kuwa hivyo, wakati hawajawa hivyo, moyoni mwao. Wanawake wengi hufanya kitu hicho hicho. Huwa hatuwaambii kuwa yawapasa kufanya hilo. Huwa tunawapa tu utaratibu. Uwaambie kile Biblia inachosema, na kama wamezaliwa kwa Roho wa Mbinguni, basi roho yao siyo ya Kiamerika tena, siyo ya Kijerumani tena. Ni ya Kimbinguni, penye, Ufalme wa Mungu. Kwa sababu tuko katika Ufalme mwingine, Ufalme wa Mungu, ambapo unakaa uadilifu, utakatifu na nguvu.

19 30

Tunayo njia ya kuukaribia Mfalme wetu. Tunakuwa na mahojiano na Yeye tunapotaka kumwita Yeye. Hatuna waombezi wengine, hatuna mpatanishi mwingine katika ya Mfalme na sisi, isipokuwa yule Mtu mmoja, Kristo Yesu. Hivyo tunaishi katika Ufalme. Na Huo unaitwa, katika mpangilio wa matukio katika Biblia, “wa Kimasihi, Ufalme wa Kimasihi.” Kwa maneno mengine, pale Masihi anapotawala katika kila maisha katika utawala Wake, akitawala maisha ya watu Wake, watu walioitwa kutoka kwenye kila mtindo wa maisha, akiwakusanya pamoja katika kundi, na kuliita Hilo, “Kanisa Lake,” “Watu

Wake walioitwa.“ Je hilo siyo jambo zuri? [Kusanyiko linasema, ”Amina.“-Mh.]

20 31

Sasa, Israeli walikuwa watu wa Mungu hadi (tunakuta katika Matendo 7:38, kama mnaliandika hilo) kuwa wakati huo wao waliitwa kanisa la Mungu, kwa sababu wao waliitwa na Mungu, watoke Misri, kutoka ulimwenguni, watoke nje mbali na makanisa mengine, watoke nje mbali na dini nyingine, ili watembee pamoja na Mungu pekee.

Na, sasa, Kanisa la Mungu leo ni kitu kile kile, limeitwa litoke nje ya kila kitu cha ulimwengu, limeitwa litoke nje ya kila kundi la kidini, limeitwa litoke nje ya kila dhehebu la kidini, limeitwa litoke nje ya kila shirika la kidini, ili kufanya kazi pamoja na Mungu. Siyo kutawaliwa na askofu, isipokuwa kutawaliwa na Kristo, katika huu Ufalme wa Kimasihi tunaoishi ndani yake. Kristo ni Mfalme. Kristo Ndiye.

21 Sasa, Kristo ni Kichwa cha Huu. Kristo ni Kichwa cha huu Ufalme wa Kimasihi. Na huwezi kufanya kuwa shirika Ufalme ambao Kristo ndiye Kichwa. Huwezi kufanya kuwa dhehebu Ufalme ambao Kristo ndiye Kichwa.

Kwa sababu, Kristo ni Mfalme, na wewe huwezi kuchukua akili za mwanadamu na kuunda shirika ambalo Kristo atalitawala. Kwa hiyo, makampuni yoyote, watu wowote, makundi yoyote ya watu, yanayojaribu kuundia shirika Ufalme wa Mungu, yanakwenda kinyume na Mfalme. Hivyo ikiwa liko dhidi ya Mfalme, litakuwa kinyume na Mfalme. Na kama linakwenda kinyume na Mfalme, litakuwa dhidi ya Mfalme. Hivyo kama liko kinyume na Mfalme, litakuwa mpinga-Kristo. Hilo ni la kali hasa. Ninayo sauti ndogo zaidi, tutalifafanua hilo. Ni mpinga-Kristo. Na kama mtanivumilia kwa dakika chache, nitalithibitisha hilo. Roho ya mpinga-Kristo hujaribu kukuwachukua watu na kuwaita kutoka shirika kwenda kwenye shirika, ikiwafanya wao kuwa shirika pamoja, ambapo kamwe haikuwa mapenzi ya Mungu. Watu siku zote wamenilalamikia kwa sababu huwa nayagonga mashirika kwa nguvu mno. Siyo watu walioko ndani humo, ambao ninawagonga. Ni ile roho inayounda dhehebu inayowafanya watu wafikiri kwamba, “Sisi ndiyo watu wenyewe.”

22 34

Watu wa Mungu ni watu Wake walioitwa watoke. Naamini wao wako katika kila dhehebu. Wangeweza kuwa Katoliki. Wangeweza kuwa Protestanti. angeweza wakawa Wayahudi. Wangeweza wakawa aina yoyote ya kanisa. Lakini Kanisa halisi ni Mwili wa siri wa Yesu Kristo.

Sasa, huwezi kuundia shirika Mwili wa siri wa Kristo. Sasa, kila mtu ajaye kwa Kristo, hutoka kwenye ulimwengu, huja ndani ya Kristo, huja ndani ya Mwili Wake wa siri. Na wewe ni mshirika wa huo Mwili unapoletwa katika hili Kanisa, uliyeitwa na kubatizwa katika huu Mwili wa siri. Mnalielewa hilo? Siyo Methodisti, siyo Baptisti, siyo Pentekoste, siyo Nazareti, siyo Pilgrim Holiness, siyo Katoliki; isipokuwa Mwili wa Yesu Kristo. Tutalichukua hilo kwa kilindi kidogo katika maswali mengine, katika dakika chache zijazo, tunapoendelea katika sehemu za kilindi za hilo. Lakini, Mwili wa Kristo ni Kanisa.

23 36

Sasa, Yeye aliufananisha Huo katika mifano mingi, kama katika mume na mke. Yeye huita Kanisa, "Bibiarusi." Na bibiarusi hayupo tena, na bwanaarusi hayupo tena, watu wawili; wao ni mmoja. "Yeye ni nyama ya nyama yake na mfupa wa mfupa wake." Na ndipo wakati mwanamume au mwanamke anapoitwa kwenye Mwili wa siri wa Kristo, kwa njia ya Roho Mtakatifu, wao wanafanyika kuwa kiungo kamili cha huu Mwili wanapokuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu. Bila shaka, Mungu alichukua Roho kutoka kwa Kristo, akaufufua mwili Wake na kuuweka huo juu ya Kiti Chake cha Enzi, na kumtuma Roho Mtakatifu kuunda ule Mwili wa siri wa Kristo, ambao utaunganishwa kwenye Karamu ya Harusi kwenye Kuja kwa Bwana. Huwezi kuuunda Huo kuwa shirika. Ni fumbo.

24 37

Yesu alimwambia Nikodemu, "Upepo huvuma unakoelekea. Wewe huwezi kujua unatokea wapi au unakwenda wapi. Vivyo hivyo kwa kila mmoja aliyezaliwa kwa Roho." Huwezi kumwelewa Huyo. Yeye anatokea mahali fulani.Na siyo Methodisti. Siyo Baptisti. Siyo Pentekoste. Siyo shirika lolote. Ni Kuzaliwa, aliyezaliwa katika Ufalme wa Mungu.

38

Sasa, kujaribu kuuunda Huo kuwa shirika, basi huleta hilo kwa mpingaKristo, kwa sababu chochote kilicho dhidi ya fundisho la Kristo ni mpingaKristo.

25 Sasa, hili shirika lilianzia wapi wakati huo? Yesu, Yeye alipokuwa duniani, hakuwahi kuunda shirika lolote la kanisa. Yeye alinena juu ya Kanisa linalokuja, lakini kamwe hakuunda shirika lolote la kanisa. Hapakuwepo kamwe kanisa lililofanyika kuwa shirika, kwa miaka mamia baada ya kifo cha mtume wa mwisho. Na kanisa la kwanza kufanyika shirika lililowahi kuwepo duniani, lilikuwa kanisa la Katoliki la Rumi. Sasa, ninacho Akina Baba Kabla Ya Nikea, Kitabu cha Wafia Dini cha Foxe, maandishi ya Josephus, Vipindi Vya Kwanza cha Pemberman, na vingi vya waandishi wa kale. Na hakuna popote, hakuna popote palipowahi kuandikwa kwenye ukurasa wowote wa historia, ambapo paliwahi kuwepo na kanisa lililofanyika kuwa shirika hadi kanisa la Katoliki la Rumi lilipofanyika kuwa shirika. Na hilo likafanyika kuwa shirika, ambapo ni kinyume na Mungu.

Sasa, kama kitu kama hiki kilikuwa kinakuja ... Ee, natamani ningeweza kuwaingizia hili mioyoni mwenu. Kama kitu kama hiki kilikuwa kinakuja, na kingekuwa mpinga-Kristo mkuu namna hii, je Mungu hangetangulia kulijua hilo, kama Yeye ni Mungu asiye na mwisho? [Kusanyiko linasema, "Amina."Mh.] Yeye hana mwisho. Je, Yeye hangelijua kwamba haya mambo yalikuwa yanakuja? Na kama ni kitu cha kutisha kama hiki, je Yeye hangelionya Kanisa Lake mapema? ["Amina."] Sasa, natumaini mnao ufahamu ulio bora zaidi kwa nini huwa nagonga, siyo watu katika mashirika ya dini, bali mashirika ya dini katika mpangilio wake. Haliwezi kuwa kitu kingine chochote isipokuwa mpinga-Kristo, katika kila moja ya hayo.

26 Sasa unasema, "Subiri kidogo, nilifikiri hukuhubiri chochote bali Biblia."

Hebu tuiachie Biblia iseme hilo, basi. Ebu tufungue sasa na tusome kidogo. Fungueni pamoja na mimi kwenye Ufunuo, sura ya 17. Huu ni ufunuo wa Yesu Kristo, kwa Kanisa Lake, Kanisa lililoitwa. Ufunuo 17. Na tutajaribu kulifanya hili kwa haraka tu iwezekanavyo. Lakini sasa uwe mwangalifu tunaposoma.

... akaja mmoja wa wale malaika saba, wenye vile vitasa saba, akanena nami, akisema, ... Njoo huku; nitakuonyesha hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi:

Sasa, hili lote ni kwa mfano, kwa sababu ni ufunuo wa Yesu Kristo, uliotiwa lakiri.

Je, mlijua hilo? Ni kitu kilichofichwa, na kinaweza tu kufunuliwa, siyo kwa wazo la kiakili, bali kinafunuliwa kwa Roho Mtakatifu kupitia karama za Roho. "Kwa yeye aliye na hekima aihesabu ile tarakimu ya huyo mnyama. Kwa yeye aliye na hekima, karama ya hekima, hebu yeye afanye hili na yeye afanye hilo." Na huu ndio ufunuo wenyewe.

27 43

Sasa, mtu yeyote anajua kwamba mwanamke anapokuwa mfano katika Biblia, inahusiana na kanisa. Kanisa la Kristo linaitwa "Bibiarusi." Paulo alisema, "Nakuposea wewe kwa Kristo kama bikira safi."

44

Sasa hapa tunanena juu ya mwanamke mkuu ambaye ni mwanamke mwenye sifa mbaya. Malaika alimwambia Yohana, "Njoo huku, nitakuonyesha," "hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi." Sasa, "mwanamke aketiye juu ya maji mengi," linaonekana kama fumbo, lakini lote liko hapa. Biblia inalielezea hilo.

Sasa hebu tufungue kwenye sura ya 15, ili tuweze ... au aya ya 15, nadhani, ya sura hiyo hiyo, hivyo unaweza kuona kile "maji" yanachomaanisha.

Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa, ... makutano, ... na mataifa, na lugha.

28 45

Kwa hiyo, yale maji ambayo yule mwanamke alikuwa ameketi juu yake, huko, alikuwa na udhibiti juu ya "mataifa, jamaa, makutano, na lugha." Yeye alidhibiti lote hilo; mwanamke, mwanamke mwenye sifa mbaya.

Sasa, kama mwanamke ni mwenye sifa mbaya, kama tunamjua mwanamke alikuwa anaitwa hivyo kwa asili, kwa mwanamke, tungejua kwamba yeye alikuwa siyo mkweli kwa mume wake. Hicho ndicho yeye angeitwa. Ndipo yeye angekuwa anajifanya kuishi kwa uaminifu kwa mwanamume, na huku akiishi bila uaminifu kwake. Je, hilo ni sahihi? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.]

Vema, basi, hili ndilo kanisa linalosema kwamba Kristo ni Mume wake, na mafundisho ya kanisa hilo yakiwa kinyume na Fundisho Lake. Yeye ni kahaba. Na yeye anadhibiti watu na makutano na mataifa. "Njoo huku na nitakuonyesha hukumu yake." Sasa tumepata ile picha.

29 ... ambaye wafalme wa dunia wamezini naye, nao wakaao katika nchi ... wamelevywa kwa mvinyo ya uasherati wake.

46

Uasherati ni nini? "Unajisi; kuwa mchafu." Yeye ni kahaba. Yeye ni mchafu, na watu wote matajiri wa ulimwengu, wafalme na watu wakuu wa mataifa na makutano, wamefanya naye uasherati, wameshiriki uovu wake. Mnaona kule linakoelekea, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Unaona?

30 47

Sasa, mimi siwajibiki kwa kuandika Hili, lakini nawajibika kama silifundishi Hilo. Loo. Tunazungumza kuhusu kanisa sasa. Sasa, kama mtaona, tunapoendelea mbele kidogo.

Akanichukua katika Roho hata jangwani: nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana, ...

48

Hebu nichukue hii mifano tunapoendelea. Sasa, nyekundu kama damu ni "nyekundu." Nyekundu, kwa njia moja, ni rangi nzuri. Nyekundu, kwa njia nyingine, ni rangi yenye sifa mbaya, mwanga mwekundu, rangi ya hatari, rangi nyekundu kama damu. "Alikuwa amepambwa kwa rangi nyekundu kama damu," nyekundu, kahaba.

49

"Na alikuwa ameketi juu ya mnyama." Mnyama, katika Biblia, humaanisha, "nguvu." Kama mtaona, wahudumu wengi, nawaona wakitikisa vichwa vyao, sawa, kwa sababu wao ni walimu wa Biblia. Mnyama humaanisha "nguvu." Tunawaona hawa wanyama wa kwenye-wa kwenye Biblia, wa Ufunuo 13, na wa Danieli, wakija kutoka

kwenye maji; wanyama, nguvu, wakija kutoka miongoni mwa watu.

31 50

Lakini mliona? Katika Ufunuo 13, wakati Amerika inapoinuka, ndiyo mnyama pekee katika Biblia, anayeinuka, ambaye hakutoka kwenye maji. Biblia ilisema hiyo ilitoka katika nchi, ambapo hapakuwepo na watu. Huo ulikuwa huu ufalme mpya. Na alionekana kama mwanakondoo, lakini baada ya kitambo alinena kama joka. Hiyo ni hii nchi. Inapasa hilo litukie. Siku fulani watafanya makosa na kumchagua mtu asiyefaa. Watamwinua Yusufu, au ... "Farao ambaye hamjui Yusufu." Walijaribu hilo hapo kabla, nao watalifanya hilo tena, kama wakishindwa wakati huu.Hatimaye hilo litakuja. Biblia inasema hivyo. Mimi siyo mwanasiasa. Pande zake zote mbili zimepotoka. Mimi napiga kura yangu kwa Yesu Kristo. Yeye Ndiye pekee ninayemhitaji. Lakini, nawaambia, ni bora mweke mambo sawa sasa, mtarajie uhuru wowote kwa ajili ya watoto wenu. Sijui liko karibu kiasi gani. Ombeni. Vema. Kuwa na ...

32 Tazama.

Akanichukua katika Roho hata jangwani: nikaona mwanamke (kanisa), ameketi juu ya mnyama mwekundu sana,mnyama mwekundu sana, mwenye kujaa majina yenye makufuru, mwenye vichwa saba na pembe kumi.

51

"Vichwa saba." Chini hapa, Hilo lilisema, "Vile vichwa saba," ambavyo vilikuwa juu ya yule mnyama, "ni vilima saba ambavyo ule-ule mji unakaa." Sasa ni mji gani uliojengwa juu ya milima saba? [Kusanyiko linasema, "Rumi."-Mh.] Rumi, kabisa, mji ukaao juu ya vilima saba; kanisa, mwanamke, kahaba ambaye atadhibiti ulimwengu kwa nguvu zake. Mbona, ni wazi tu kama vile kusoma gazeti. Unaona? Hakika.

33 Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu sana, (yule mwanamke, kanisa, tajiri), amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, ...

52

Niambieni ni wapi mojawapo liliwahi kulipa kodi. Niambieni ni wapi wamelipishwa kodi kwa chochote. Wanayo haki juu ya chochote wanachotaka kufanya. Na bado, Mungu anao watoto ndani mle. Hakika anao.

53

Ni hivyo hivyo, chungu hakiwezi kuiambia birika kuwa ni nyesu. Wakati mwingi, Waprotestanti husema, "Vema, Wakatoliki, walimwua huyu, yule, yule mwingine." Ni nani aliyemwua Joseph Smith? Sikubaliani na yeye. Lakini yeye alikuwa tu na haki kwa ajili ya fundisho lake kama nilivyo nayo kwa ajili ya la kwangu, hapa katika Amerika. Na kanisa la Methodisti lilimwua Joseph Smith. Unapokuja katika-Salt Lake City, pana ishara kuu kubwa, "Ninyi Wamethodisti, kaeni macho na senene wa Mormon." Sawa. Kanisa la Methodisti lilimpiga risasi Joseph Smith. Waprotestant! Hivyo, usipige kelele kuhusu Katoliki. Angalia, kwa dakika chache tu, Biblia itasema hivyo, pia.

34 ... na kito cha thamani ... na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake, mafundisho yake ya imani, kile yeye alichokuwa akikitoa, wafalme wa dunia wakinywa hicho.

54

Mtu yeyote angeweza kuamini hilo, angeweza kuamini vidonge vya vitamini vya Ndugu Jagger, kwamba, "Unaweza kunyunyizia maji juu ya mwanamke aliyeolewa na mwanamume kwa miaka thelathini, na amekuwa na kundi la watoto, na kumrejesha kuwa bikira na kumpeleka kwenye kitanda cha bibiarusi usiku huo pamoja na mume wake." Mtu yeyote ambaye angeweza kuamini yale maji matakatifu yatafanya hilo, anaweza kuamini chochote. Hiyo ni sahihi.

Lakini wafalme wa nchi wanatenda mambo kama hayo. Ni kwamba waweze kuishi na kuwa na hali ya kujisikia amani. Chini moyoni mwako unajua kuwa umeoza. Inahitaji Damu ya Yesu Kristo kukutakasa. Lakini sasa tazama, hilo lilikuwa kanisa la kwanza lililoundwa kuwa shirika, Biblia inanena juu yake hapa.

35 Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, BABELI MKUU, YA FUMBO, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.

Sasa angalieni. Sote tutakubaliana. Na vitabu vya Rumi yenyewe, vitabu vya Katoliki yenyewe, vinakubali kwamba hilo ni kanisa Katoliki. Vitabu vyao wenyewe vinakubaliana na hilo. Ninacho kitabu kinachoitwa Kweli Za Imani Yetu, kinakuwa cha kasisi pekee. Mkatoliki aliongoka kwenye ... Ambaye, mtoto wake wa kiume alikuwa kasisi, na yule mama akanipa kile kitabu. Ndipo yule kasisi akamtaka mama akirudishe kanisani; akaja kukichukua, nami sikumruhusu akichukue. Nilikiweka hicho kwa ushahidi, nilitaka kujua kile nilichokuwa ninakizungumzia. Ninaposema lolote, ni lazima nilijue hilo. Mungu anakwenda kuniwajibisha kwa ajili ya hilo.

36 56

Na kumbukeni, yeye aliitwa "BABELI YA FUMBO." Tunajua hilo ni kanisa Katoliki. Lakini, tazama, hilo ni, "MAMA WA MAKAHABA."

Kahaba ni nini? Kitu kile kile hilo lilicho, kahaba. Sasa, haya mashirika ya dini yalitokea wapi? Huyo hapo mama yao. Hicho ndicho hayo yalicho, kwa kuanzia. Ndipo unasema, "Huyo ni mpinga-Kristo." Hiyo ni kweli. Basi kama huyo ni mpinga-Kristo, basi vipi kuhusu mashirika yetu ya dini? Kama tu kahaba na changudoa, ni kitu kile kile, "akifanya uzinzi, akifanya uasherati," likipokea mambo ya uongo kwa sababu ya mambo ya kiakili na kisomi ya wanadamu." Kama Biblia ilivyosema, "Wakifanya maagizo ya wanadamu kuwa ndiyo Mafundisho ya imani. Hilo ndilo linaloitwa kanisa leo hii, ambalo liko kinyume na Ufalme wa Mungu.

37 57

Kama katika Agano la Kale. Mungu alitaka kuwa Mfalme juu ya Israeli, kabla halijafanyika kuwa kanisa, na Yeye alikuwa Mfalme. Na ingawa wao walikuwa na nabii, Samweli, mtu mwema, na yeye alipokuwa amewaambia hilo, kama wao walihitaji mfalme, lakini wao walitaka kuwa kama wale watu wengine. Wao walitaka kuwa kama Wafilisti.

Hilo ndilo tatizo la watu walio Waprotestanti. Hawataliruhusu tu lililo jema vya kutosha. Wao tu ... Wakati Roho Mtakatifu aliposhuka juu yao nyuma huko, miaka arobaini iliyopita, na nguvu zikaanza kuwamwagikia, nao wakaanza kucheza na kupiga kelele, na kunena kwa lugha. Wao hawakuachia hilo peke yake. Iliwapasa kulifanya hilo kuwa shirika la dini. Ndipo likaja moja, na wakawaita Baraza Kuu. Likaja lingine, likiwa na Nuru kidogo kwenye Jina la Yesu Kristo, na wakawaita hao "Mambo mapya" na kuwatoa nje. Ndipo likaja shirika la dini liitwalo P.A. ya J.C., Makusanyiko ya Kipentekoste ya Yesu Kristo. Msuguano mdogo ukaja kati yao, kama Yeye amekuja akiwa juu ya farasi mweupe au jinsi Yeye alivyokuwa aje, nao wakaunda shirika lingine la dini, lililoitwa P.A. ya W., Makusanyiko ya Kipentekoste ya Ulimwengu. Loo, jamani, jamani! Ndipo likaja kanisa la Mungu. Halafu wakavunjika kwa njia ya unabii, wakaunda shirika la dini tena. Kila wakati unapolifanya hilo, unatoka nje ya mapenzi ya Mungu. Roho ya mpinga-Kristo.

38 59

Kanisa la Mungu liko huru. Kanisa la Mungu halijawekewa mipaka yoyote, kwa sababu, kutokea bahari hadi bahari ni ya Mungu, kila mwanadamu chini ya nchi ni Wake. Kama yeye alikuwa katika Katoliki, Protestanti, au chochote kile yeye alicho, Mungu hutafuta wale walio na moyo mnyofu. Na tunaokolewa kwa imani, kwa kumwamini Yeye. Hilo ndilo Kanisa. Sasa, unaona, Kanisa siyo shirika la dini.

60

Na kila wakati unapoona shirika la dini, kumbuka tu, "mpinga-Kristo" imeandikwa juu yake. Liko hapa katika Biblia. Hilo liko wazi kadiri nijuavyo jinsi ya kulisoma Hilo. Nininao wengi wa marafiki wa thamani walioketi hapa, ambo ni wa mashirika ya dini, sisemi ninyi ni mpinga-Kristo. Mimi siwaiti hilo. Lakini nyuma ya hilo jambo lote, na inaonekana kana kwamba Shetani amelipindisha hilo kwa namna ambayo hadi inakupasa kuwa na kitu fulani kama hicho au hata hawatakuruhusu uhubiri.

Ndicho kitu kile kile mataifa yalicho nacho. Huwezi kuwa mtu bila kuwa na taifa. Inakupasa kuwa na taifa mahali fulani. Inakupasa ama kuwa Mwamerika, Mjerumani, au kitu fulani. Unaona, lote limepindishwa tu.

39 Hivyo, kwa kweli, Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili ni kama msafiri. Mbele ya ulimwengu yeye ni mwasi. Lakini mbele ya Mungu yeye ni wa thamani. Natamani

tungekuwa na muda kwenda kwenye Waebrania 11, na tuone (jinsi) wale mashujaa wa imani. Jinsi Abrahamu alivyotoka nje na kujiita mwenyewe msafiri na mgeni, akasema ulimwengu huu ulikuwa nyumbani kwake, lakini yeye alikuwa anasafiri, akitafuta Mji ambao mwenye kuujenga na kuuunda alikuwa Mungu. "Na kama sisi, tukiwa tumekufa katika Kristo, tunachukua Uzao wa Abrahamu, na ni warithi Kwake, kwa ahadi." Na hilo linatufanya kuwa nini? Mahujaji na wasafiri.

40 62

Wakati Israeli walipotoka Misri. Ilikuwepo Moabu, nchi kuu iliyokuwa na utaratibu. Alikuweko pia Esau, nchi kuu iliyokuwa na utaratibu. Na hapa kuna Israeli, wasio wa kidhehebu, wakija. Wote hao wakiwa kimsingi katika Neno. Kumbukeni, Balaamu alitoa dhabihu ile ile ambayo Israeli walitoa, madhabahu saba, jinsi Mungu alivyohitaji. Dhabihu saba zilizotakaswa, kondoo dume saba, zilizonena juu ya kuja kwa yule Mmoja Mwenye Haki. Kimsingi, wote wawili walikuwa sahihi, tukinena kimsingi. Lakini kile Balaamu alichoshindwa kuona, yeye alishindwa kuona lile la Kiungu miongoni mwa Israeli, lile kundi lisilo la kidhehebu. Hakuna mahali pa kwenda, walikuwa wanasafiri, lakini walikuwa njiani mwao mahali fulani.

Hivyo ndivyo Kanisa la Mungu aliye hai lilivyo leo hii. Hilo siyo shirika la dini, kulingana na hali ilivyo. Lakini hilo limeshikiliwa pamoja, siyo kwa kufungwa na ushirika wa dini, isipokuwa kwa nguvu na Roho wa Yesu Kristo, kwa kifungo cha upendo.

41 64

Humfanya Mmethodisti na Mbaptisti kila mmoja akimpigapiga mwenzake mgongoni, na kusema, "Ndugu yangu wa thamani," wakati wanaona hawawezi kutembea pamoja hadi wakubaliane.

Watu husema, "Je, wewe ni Mkristo?"

65

"Mimi ni Mbaptisti." Hilo halijibu hilo swali, hata kidogo. "Je, mimi ni Mkristo? Mimi ni Mpentekoste." Hilo halijibu hilo swali.

66

Kama wewe ni Mkristo, wewe ni kiumbe kilichozaliwa upya. Wewe uko ndani-ndani ya Ufalme wa Mungu wa siri. Macho yako hayako kwenye vitu vya ulimwengu bali kwenye vitu vya juu. Na hapo ni wakati wewe upo ndani ya Kanisa. Hilo ni Kanisa. Hilo siyo shirika la dini. Kamwe haliwezi kuwa shirika la dini. Niweke katika kumbukumbu. Kanisa la Mungu aliye hai kamwe haliwezi kuwa kundi lolote fulani. Haliwezi kuwa shirika la dini. Inapasa liwe Mwili wa siri, Roho Mtakatifu. Tutaendelea mbele kidogo, kama tutapata muda, tutaingia moja kwa moja katika hilo.

42 67

Sasa, mnaona kile Kanisa linachomaanisha? Kanisa humaanisha kundi "lililoitwa litoke," watu walioitwa watoke wale wanaotawaliwa tu na Mfalme wa huu Ufalme wa Kimasihi pekee. Ee, je, hilo siyo zuri? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh] Nalipenda hilo. Niliposoma hilo kwenye ... leo hii. Na liliposema pale, "Ufalme, Himaya ya Kimasihi." Mwandishi aliliweka, "Himaya ya Kimasihi." Mwandishi pia alisema, "Hakuna kitu kama Kanisa la Mungu aliye hai lililowahi kufanyika kuwa shirika la dini. Shirika ni kitu fulani kilichorekebishwa, kilichopangwa na kukubaliwa, ili kuchukua mahali pa kingine."

43 68

Hivyo ndivyo hasa jinsi haya mafundisho ya uwongo yalivyoingizwa ndani, ili kuchukua mahali pa lililo halisi. Hiyo ndiyo sababu huyo mwanamke alikuwa na kikombe cha uchafu wa machukizo yake. Sasa, unaona, sisemi ... Wapentekoste wana hatia tu kama Katoliki, au Pilgrim Holiness, au Wanazareti, au Wabaptisti, au Wamethodisti. Lakini, katika hayo makanisa yote ya kidhehebu, Mungu anao watoto. Wao ni wa huu Ufalme wa siri. Kitu pekee wao wanachokisubiri ni kuona jambo fulani likitukia, ambalo litavuta mioyo yao kuingia ndani ya hilo. Ninafurahi mno kujua, usiku huu, kwamba wao wanatoka mashariki na magharibi, kaskazini na kusini, wakijivuta wenyewe watoke, wakiabudu, wakisubiri Kuja kwa Bwana. Biblia lilisema wao wangefanya hilo katika siku za mwisho. Hiyo ni sahihi kabisa. Na ilisema, "Wangelitembea kutoka mashariki kwenda magharibi, kaskazini na kusini, wakitafuta Neno la kweli la Mungu; siyo njaa ya mkate na maji, bali kwa ajili ya kusikia Neno la Mungu."

69

Wanataka wewe, "Njoo jiunge na hili. Njoo jiunge na hili." Hakuna chochote unachojiunga nacho. Katika Ufalme wa Mungu, hakuna kitu hata kimoja unachoweza kujiunga nacho. Ni tendo binafsi la kuzaliwa kwenye Kanisa, siyo kujiunga kwenye Hilo. Sasa, huenda nikawa na mengine zaidi kidogo ya kueleza juu ya hilo, katika dakika moja. Ninayo Maandiko zaidi niliyoandika chini hapa.

44 Lakini sasa hebu twende kwenye wazo la pili, hivyo tuweze kujaribu kupitia lote hilo. Ni nani aliyeuweka huo, yaani, huu Mwili wa siri? Ni nani aliyeuanzisha Huu? Yesu Kristo. Na ni ... Yeye ni Kichwa cha huu Mwili wa siri. Yeye ndiye Mfalme juu yake, akifanya mapenzi Yake Mwenyewe katika Utawala Wake. Siyo udhibiti wa askofu au udhibiti wa baraza la kanisa: bali Mfalme, ambaye ni Masihi Mwenyewe akifanya kazi katika Utawala Wake Mwenyewe. Hilo lilianza lini? Kwenye Pentekoste. Siyo shirika la dini la Kipentekoste: uzoefu binafsi wa Kipentekoste. Huo ndiyo wakati hilo lilipoanza kwako. Yeye alinena juu ya kuja kwa Hilo. Yeye alisema kile ambacho kingetukia. Yeye alisema Hilo lilikuwa linakuja.

45 71

Sasa, kama tunapenda, tunaweza kufungua kwenye Luka, sura ya 24, aya ya 49, na tunaweza kuona hapa, tuanze kusoma baadhi ya Maandiko ili watu hawa wanaochukua hili waweze kuliandika. Lika 24:49, tutaona kile Yeye alichosema:

Na, tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu, lakini kaeni katika mji wa Yerusalemu, hata mvikwe uwezo utokao juu.

72

Sasa, Yeye aliahidi Kanisa ambalo lingekuja, Ufalme ambao ungekuja. Sasa fungueni moja kwa moja kwenye Matendo 1:8. Sasa, kumbukeni, Yeye alinena pia katika Mathayo 16:18, kuhusu, "Juu ya mwamba huu," Yeye angelijenga Kanisa Lake, "na malango ya kuzimu hayangelilishinda Hilo." Tunakwenda kufikia hilo katika dakika chache tu zijazo, tunapoendelea chini katika somo lingine. Matendo 1:8.

Lakini mtapokea nguvu, akiisha ... kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu: nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, ... na katika Uyahudi, ... na Samaria, na hata pande za mwisho kabisa za ulimwengu.

73

Ufalme unaokuja wa mashahidi, mashahidi wa ufufuo Wake, mashahidi wa nguvu Zake, mashahidi wa Yeye kuwa hai. "Ninyi ni mashahidi Wangu," sasa, Matendo 1:8.

46 74

Basi tunakuta hilo pia katika Waefeso, sura ya 1, aya ya 22, ninyi mnaoandika hilo. Kuna mengi tu hayo ambayo mtayaandika, lakini ili tu kuligongea hilo chini ndani yenu, ili kuhakikisha kuwa mna ... mnaliona hilo. Vema. Ile aya ya 22 ya Waefeso, sura ya 1.

Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake (huyo ni Kristo), akamweka Yeye awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa,

Ambalo ndilo mwili wake, na utimilifu wa Yeye aliyevijaza vitu vyote ndani ya wote.

75

Ni nani aliyeliweka katika nafasi yake hili Kanisa? Yesu Kristo. Hakuna askofu, hakuna kundi la watu, hakuna papa, hakuna nguvu zilizoundwa na mwanadamu, hata kidogo. Lakini Yesu Kristo alinena juu ya Hilo likiwa Ufalme Wake uliokuwa unakuja katika nguvu. "Baadhi husimama hapa ..." Sura ya 16 ya Mathayo, "Amin, nawaambieni, pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapoona Ufalme wa Mungu ukija katika nguvu." Siku chache tu baada ya hilo, Yeye alisulubishwa, na Roho Mtakatifu akashuka. "Baadhi wamesimama hapa, hawataona mauti hadi waone Ufalme wa Mungu."

47 76

Wayahudi wakamwuliza Yeye, "Je, Wewe utaurejesha Ufalme wakati huu?"

Yeye alisema, "Si kazi yenu kujua wakati au majira, Baba aliloliweka katika nia Yake Mwenyewe." Matendo 1, "Mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu." Mtapokea nguvu, ukiisha kufanywa askofu, ukiisha kufanywa mhubiri,

ukiisha kufanywa papa, ukiisha kufanywa kasisi? "Mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu." Huyo ndiye shahidi ambaye Mungu alikuwa anamtafuta, shahidi baada ya kuja kwa Roho Mtakatifu. Siyo shahidi kwamba mimi ni askofu, siyo shahidi kwamba mimi ni mchungaji. Bali shahidi (wa nini?) wa Mfalme aliyefufuka. Hilo ndilo Kanisa la kweli la Mungu aliye hai. Vema.

48 78

Na pia katika Wakolosai 1:17 na 18, tunaweza kusoma hili tu tunapokuwa kwenye hilo. Wakolosai 1:17 na aya ya 18.

Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na kwa njia ya Yeye vitu vyote hushikana.

Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa:ambaye ni, ambaye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza kutoka kwa wafu; ili kwamba awe mtangulizi katika mambo yote.

79

Ni nani aliye Kichwa cha hili Kanisa? Yesu Kristo. Ni Ufalme gani? Ufalme wa Kimasihi, Kanisa, siyo shirika la dini; Kanisa, Mwili wa siri ambao Kristo ndiye Kichwa Chake. Loo, nalipenda hilo, kutembea katika Roho, ukimtii Mfalme. Ukiwa mpumbavu kwa ulimwengu; ukiwa wa thamani mbele za Mungu. Ukitembea katika Roho; hueleweki, unachekwa, unadhihakiwa. "Wale wote waishio kitakatifu ndani ya Kristo Yesu watateswa. Kama wao waliwatesa manabii waliokuwa kabla yenu, wakamwita Mkuu wa-Mkuu wa nyumba, 'Beelzebuli,' si zaidi sana watawaita ninyi wanafunzi Wake?" Lakini mnatembea katika Roho, mkigeuzia kisogo kwenye mambo ya ulimwengu, siyo mliofungwa pingu zozote." "Yeye ambaye Mwana amemweka huru yuko huru kweli kweli." Amina.Hilo ndilo Kanisa la Mungu aliye hai. Huyo Ndiye aliyeliweka Hilo.

49 80

Sasa tunaona, katika mashahidi, katika Matendo 1:8, Yeye alisema,

"Mtakuwa mashahidi Wangu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu."

81

Kanisa ni nini? Ule mwili wa siri wa Kristo. Ni nani aliyeuweka? Bwana Yesu, Mwenyewe. Haukuanzishwa kule Rumi. Wala hakuanzishwa katika Uingereza, na John Wesley. Wala haukuanzishwa na Calvin, au katika Amerika, Baptisti, na John Smith. Wala haukuanzishwa katika California, na Wapentekoste. Huo ulianzishwa na Yesu Kristo, Mfalme wa Ufalme wa Kimasihi. Huyo Ndiye aliyeuanzisha Huo. Yeye ni Mfalme. Yeye anataka awe Mfalme. Yeye anataka atutawale. Yeye anataka awe Bwana.

50 82

Watu humruhusu Yeye aingie ndani, wakisema, "Nitamruhusu Yeye awe Mwokozi," lakini hawamruhusu Yeye awe Bwana. Bwana humaanisha, "umiliki, utawala." "Ingia moyoni mwangu, Bwana, uniokoe na kuzimu, lakini usiniambie kile cha kufanya." Hiyo ndiyo msimamo wa watu. Hiyo ndiyo sababu. Si ajabu Biblia ilisema, "Meza zote zimejaa matapiko." Je, unajua matapishi ni nini. "Kama mbwa anavyogeukia matapishi yake." Kama haya mashirika ya dini hayakufanya kazi, katika wakati wa kwanza, na ikabidi Mungu ayatapikie mbali; ukirejea kwao, watakufanya utapike tena. Yeye alisema, "Ni bora ungekuwa moto au baridi. Kwa sababu u vuguvugu, nitakutapika kutoka kinywani Mwangu." Unamfanya Mungu ajisikie tumbo Lake kuchafuka, na Yeye anatutapika.

51 83

Niambie shirika la dini lililowahi kuanguka, likawahi kuinuka tena. Nionyeshe kwa historia pale moja lililowahi kuinuka. Mtu atainuka akiwa na huduma, Mungu atambariki huyo mtu. Jambo la kwanza unajua, yeye ataigeuza hiyo moja kwa moja na kwenda miongoni mwa watu na kuunda shirika la dini kutokana na hiyo, na hilo linaiua hiyo huduma pale pale. Angalia kote kwenye historia na uone kama kuna moja ambalo liliwahi kuinuka. Hakuna hata moja, kwa sababu lote ni roho ya mpinga-Kristo miongoni mwa watu.

52 84

Kama Musa, na wengine walitaka kitu fulani ambacho wangeweza kufanya wenyewe. "Bwana, tumekuwa na washirika wengi mno mwaka huu." Inaleta tofauti gani, kwamba una washirika wangapi? Hatutafuti washirika wa kanisa. Tunatafuta washirika

wa Mwili wa Kristo, ambao wamezaliwa katika Ufalme wa Mungu, "siyo kwa mapenzi ya mwanadamu, bali kwa mapenzi ya Mungu," siyo kwa roho ya mwanadamu au akili ya mwanadamu.

85

Paulo alisema, "Kamwe sikuja kwenu pamoja na hekima ya mwanadamu. Nimekuja kwenu pamoja na Roho wa Mungu na nguvu za kufufuka Kwake, kwamba imani yenu isikae katika hekima au ufasaha wa maneno ya mwanadamu, bali katika nguvu za ufufuo wa Yesu Kristo." Hilo ndilo Yeye aliloingia nalo ndani. Mungu tusaidie, ili tufanye jambo hilo hilo.

53 86

Sasa, hatutaki kutumia muda mwingi mno juu ya kila moja. Sasa nataka kuona: Ni nini Ujumbe wa hili Kanisa? Hili Kanisa linapasa kufundisha nini? Ujumbe Wake ni nini?

Ujumbe wa kwanza ninaoweza kuuwazia, ambao hili Kanisa (Mwili wa siri) litafundisha, utakuwa toba. Hebu tufungue Luka 24 tena, kwa kitambo tu. Luka, sura ya 24. Jambo la kwanza litakachofanya, ni kutubu, na Hilo litafundisha toba. Sasa, Yesu, akijiandaa kuondoka, hii ni sura ya mwisho, Yeye alipokuwa anajiandaa kuondoka duniani. Luka 24:46, hebu tuanze na aya ya 46.

Na akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba ilipasa Kristo ateswe na kufufuka siku ya tatu:

Na kwamba habari ya toba na ondoleo la dhambi ...

Ee, nataka hilo lizame ndani, kwa sababu nakuja kwenye jambo fulani katika dakika moja, juu ya hilo, "ondoleo la dhambi."

... toba kumwelekea Mungu na ondoleo la dhambi itahubiriwa katika Jina Lake miongoni mwa mataifa yote, kuanzia tangu Yerusalemu.

Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya.

54 87

[Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.] "... kupata mateso," Maandiko yalisema. Yeye Ndiye aliyenenwa na nabii. Yeye Ndiye Biblia yote inanena habari Zake, inahusika na Yeye. Hakika Yeye angejua kile kinachopaswa kufundishwa. Yeye angejua kile kinachopaswa kufanyika. Na Yeye alisema, "Toba na ondoleo la dhambi lazima lihubiriwe kwa mataifa yote kuwa ushuhuda, kunzia Yerusalemu."

Sasa, shirika la dini lilianzia Rumi. Kanisa lililo shirika la dini lilianzia Rumi; likaja hadi Ujerumani, kwa ajili ya Martin Luther; likaendelea hadi Uingereza, kwa ajili ya Wesley; likaendelea hadi Amerika, kwa ajili ya John Smith; California, kwa ajili ya Pentekoste.

Lakini Kanisa lilianzia huko Yerusalemu. "Toba kwa Mungu na ubatizo katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, lilianzia huko Yerusalemu. Na linge ..." "Linge," Yeye alisema, Hakusema wote wangelifikia hilo. Lingepasa kuanzia. "Hilo lingekwenda ulimwenguni kote. Hilo lingehubiriwa." Lakini liko kidogo mno. Lakini hilo ndilo Yeye alilosema, Ujumbe Wake, huo ndio Ujumbe wa Kanisa. Nionyesheni kanisa linaloufundisha Huo. Niambieni Huo uko wapi. Huwezi kuupata huo.

55 88

Sasa, Yesu ni Mfalme, ule Ujumbe wa pili. Yesu ni Mfalme, na yuko hai milele na milele. Hilo ndilo Kanisa lingefundisha. Mathayo 28:20. Yesu ni Mfalme na yu hai milele na milele. Hicho ndicho Kanisa lingefundisha Mathayo 28:20.

Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

89

Je, hilo ni sahihi? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Waebrania 13:8, "Yesu Kristo ni yule jana, leo, na hata milele." Huo ndio Ujumbe wa Kanisa: likitenda kazi Zake Yeye, likithibitisha ufufuo Wake, na kutoa shuhuda.

Sasa, Matendo 5:32, pale tunapoona kama wao walikuwa na hilo au la. Tunapofungua, Matendo, ile sura ya 5, aya ya 32.

Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, na hali kadhalika pia Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wale wamtiio.

56 90

Inapasa Yeye ashuhudiwe. Yohana 14:12, Yeye anatoa fundisho, kile ambacho Kanisa lingetenda. Katika Yohana, sura ya 14, ile ... na aya ya 12, tutaona kile hiyo inachosema. Yohana 14:12, hivyo tutasoma hilo, tulifanye rasmi. Vema. Yohana 14, na aya ya 12.

Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.

91

Huo ndio Ujumbe wa Kanisa. "Yesu Kristo yule jana, leo, na hata milele," akiishi katika Kanisa, Mfalme wa Kanisa, aliyefufuka kutoka kwa wafu. "Yeye yule, jana, leo na hata milele," akitenda matendo yale yale, akifanya mambo yale yale Yesu aliyofanya. Huo ndio Ujumbe wa Kanisa. Kama kanisa alifundishi Huo, hilo linafundisha thiolojia fulani ya uwongo. Hilo ndilo Yesu alilowaamuru wao wahubiri.

57 92

Kitakuwa kitu gani kingine? Tutajuaje kama ... Hawa watu, wao husema, "Vema, mimi ni mwamini." Hebu tuone lililokuwa agizo Lake la mwisho kwa Kanisa Lake, kwa ajili ya waaminio, Marko 16. Chukueni Marko, ile sura ya 16, na tutakuta uliokuwa Ujumbe Wake wa mwisho kwa Kanisa, na tutaona basi kama tunafuata agizo Lake. Marko 16, hebu tuanzie kwenye aya ya 14.

Baadaye akaonekana na wale kumi na mmoja, hiyo ni baada ya kufufuka Kwake, walipokuwa wakila, ...

93

Hili hapa agizo kwa Kanisa sasa, sikilizeni, lile agizo la mwisho. Tutajichunguza wenyewe, kama sisi ni waaminio, au kama tuko katika ya hili Kanisa, au la.

Baadaye akaonekana na wale kumi na mmoja, hiyo ni baada ya kufufuka Kwake, walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona baada ya ufufuo wake ... Yeye alipokwishafufuka.

58 94

Mtu fulani alikuwa amemwona Yeye. Mtu fulani alikuwa akijaribu kuwaambia wao kuhusu hilo, na wao hawakuamini. Kama hilo siyo jambo lile lile leo hii. Tunajua Yeye yuko hai, tunao ushahidi wa Roho Wake ndani yetu. Tunaona nguvu Zake zikitembea juu ya umati wa watu, na makumi ya maelfu ya watu, na kutambua mawazo yao-mawazo na mioyo kabisa tu kama Yeye alivyofanya wakati Yeye alipokuwa hapa. Kama Biblia ilivyosema, "Neno la Mungu." Na Yeye ni Neno la Mungu. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu." "Neno la Mungu lina makali zaidi, yenye nguvu zaidi kuliko upanga wenye makali kuwili, ukatao hata kufikia mafuta yaliyoko kwenye mfupa, na mtambuzi wa mawazo na makusudio ya moyo." Kristo, "Matendo niyatendayo, ninyi nanyi mtayatenda pia." Tunamwona Yeye akifanya hilo. Ni wangapi wamemwona Yeye akifanya hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."Mh.] Hakika. Tunajua Yeye hufanya hilo. Yeye anaishi hapa. Yeye yuko ndani ya mioyo yetu.

59 95

Wao hawaliamini Hilo. Wao hawakuliamini Hilo wakati huo. Wao hawaliamini Hilo sasa. Wao huamini, "Yeye alikufa, na hilo likawa limekwisha. Na tunacho kitu fulani cha kihistoria, ambacho mtu fulani aliinuka miaka michache iliyopita na kuanzisha kanisa, na kuandika katekismo, na hicho ndicho tunachokishikilia." Huo ni upagani. Sawa! Hakuna ukweli kwenye hilo. Ee, sisemi "ukweli," huyo mtu huenda amelifanya hilo. Huyo mtu huenda angeweza kuwa mnyofu wa moyo mno. Lakini Mungu hadhibiti Kanisa Lake namna hiyo. Kamwe Yeye hakutaka hilo.

60 96

Wao walipomtaka mfalme, Samweli aliwaita na kusema hili. Yeye alisema, "Nataka

niwaulize jambo fulani. Je, niliwahi kuwakosea? Je, niliwahi kuwaomba fedha yenu yoyote? Je, niliwahi kuwaambia ninyi lolote katika Jina la Bwana isipokuwa lile lililokuwa sahihi? Mungu hataki ninyi muwe na mfalme. Yeye anataka awe ndiye Mfalme wenu."

97

Yeye akasema, "Ewe Samweli, hakika, uko sahihi. Wewe ni nabii mwema. Hukuwahi kutuambia lolote isipokuwa lililo Kweli. Hukuwahi kutuomba fedha. Hayo mambo ni kweli. Lakini tunataka kuwa kama hao wengine. Tunataka mfalme, hata hivyo."

98

Samweli akasema, "Hilo linakwenda kuwasababishia matatizo ya moyo na shida. Inakwe- ... Yeye atakwenda kuwachukua wana na mabinti zenu. Yeye atakwenda kuwachafua, katika mambo yeye atakayoyafanya. Yeye atafanya hilo." Na yeye alifanya hilo. Lakini, wao walitaka mfalme.

61 99

Hivyo ndivyo wao hufanya leo hii. Ee, inatupasa tuwe na jina fulani lililoambatanishwa na sisi. Tunakwenda kuwaambia watu wanapotuuliza, "Sisi ni Methodisti, Baptisti." Semeni tu ninyi ni Wakristo, hilo ni sawa, "wanaofanana na Kristo."

... Baada ya Yeye kufufuka kutoka kwa wafu, wao hawakuamini hilo.

Akawaambia, (angalieni agizo kuu), Enendeni hadi ...

Ulimwengu kiasi gani? [Kusanyiko linasema, "Wote."-Mh.] "Loo, nilifikiri, Yerusalemu pekee." Mtu fulani alisema, "Ishara hizi zilikwenda Yerusalemu pekee."

... ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili ...

62 100

Ni wangapi mnajua Injili ni nini? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Siyo "Neno." [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake.] Paulo alisema, "Injili ilikuja kwetu siyo kwa Maneno pekee, bali kupitia nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu." Injili ni nguvu ya Mungu kulifanya Neno litende kile Hilo linachosema litafanya.

"Mkahubiri Injili, ulimwenguni mwote." Hubirini Injili kwa watu weupe pekee, au weusi tu, njano, weusi?

... kwa kila kumbe.

101

Amina. "Kila kiumbe." Mnaamini kwamba hilo humaanisha hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Nimemwona Mungu akimchanganya fahali, siku moja. Nimemwona Yeye akisababisha manyigu yasiume. Nimemwona Yeye akimfufua komba aliyekuwa amelala huku amekufa, usiku wote. "Kila kiumbe." Injili itatenda kazi juu ya kila kitu utakachoomba.

Unasema, "Hilo ni kosa, Ndugu Branham." Siyo kosa.

63 102

Yesu aliuambia mti, "Umelaaniwa. Hakuna mtu atakula kutoka kwako, tangu sasa." Na injili ilihubiriwa kwa ule mti. Amina. Loo! Najisikia wa kidini, sasa hivi.

"Kwa kila kiumbe." Amina. Kuhubiria nini? "Kila kiumbe." Ee, kama tungelikuwa tu na wakati kwa ajili ya haya mambo.

Sasa, aaminiye na kubatizwa ataokoka; ...

"Ee, naamini, nimebatizwa." Vema. Vizuri. Sawa.

Aaaminiye na kubatizwa ataokoka; ... asiyeamini atahukumiwa.

103

"Ee, nafurahi mimi ni mwamini." Subiri kidogo. "Na," na ni kiunganishi, kikiunganisha sentensi pamoja.

Na ishara hizi ...

Ee, nilifikiri hamwamini katika ishara. Hayo ni Maneno ya Yesu Kristo Mwenyewe.

Bishana Hilo na Yeye.

... ishara hizi zita- ... (Siyo, "huenda hizo; wakati mwingine hufanya.") ... zitafuatana na hao waaminio; ...

104

Sasa tunakwenda kuona kama wewe unaamini au la, tunakwenda kuona kama shirika lako la dini linaamini au la. Huenda wao wakasema wanaamini. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Mbona, wao hukataa hizo ishara?

... ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; (Kiasi gani?) Katika jina langu watatoa pepo; ...

64 105

Na ninyi msioamini uponyaji wa Kiungu, ninyi makanisa! Hili linanaswa, mnaelewa. Sizungumzi tu na ninyi. Mtu fulani mwingine anakwenda kuliskia Hilo. Unadai kwamba unamwamini Mungu, na kuamini katika agizo, kwamba kanisa lako limeagizwa kuieneza Injili? Na jambo la kwanza kabisa ni uponyaji wa Kiungu.

Ni lipi jambo la kwanza Yesu alilowaambia wanafunzi Wake alipowatuma waende huko na huko? Mathayo 10:1, "Ponyeni wagonjwa, toeni mapepo." Jambo la mwisho aliloliambia Kanisa Lake lilikuwa nini? "Ponyeni wagonjwa, toeni mapepo." Alfa na Omega; Benyamini na Rubeni; Mwanzo na Mwisho; Yeye Aliyekuwako, Ambaye Yuko, na Atakayekuja; Nyota ya Asubuhi; Shina na Mzao wa Daudi. Haleluya! Huyo ni Yeye. Ndiyo, bwana.

"Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa mapepo." Huko Yerusalemu tu? "Ulimwenguni kote, na kwa kila kiumbe." Je, hiyo ni Biblia? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Hilo ndilo Hiyo ilichosema.

Huo ndio Ujumbe wa Kanisa. "Ulimwenguni kote, kila kiumbe, Injili. Kwa kila mmoja aaminiye, ishara hizi zitafuatana naye."

65 ... jina langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya;

106

Na ninyi maskini Wanazareti mliwaita hao kundi la watu wa "lugha". Hata msingeketi pamoja na wao kanisani. Je hilo siyo baya? Mnakwenda kufanya nini mtakapofika Mbinguni? Yesu alikufa, akinena kwa lugha. Wao walisema, "Yeye alinena, na Yeye alinena katika lugha nyingine." Hakika. Yeye alinena. "Yeye alinena katika Kiebrania." Yeye hakufanya hivyo. Hayo siyo maandishi ya Kiebrania. Yeye alinena katika lugha ya Kimbinguni.

66 107

Habili alipotoa dhabihu ya mwanakondoo wake juu ya mwamba, wakati huyo mwanakondoo mdogo alipokuwa anakufa, Habili alikuwa anamkata shingoni. Mfano wa Kristo, huko nyuma katika bustani ya Edeni, huyo mwanakondoo mdogo akilia katika lugha nyingine, alipokuwa anakufa. Huyo alikuwa mfano, sufu yake iliyotapakaa damu yake mwenyewe. Huyo alikuwa mfano wa Mwana wa Mungu akining'inia kule Kalvari, akakatwa vipandevipande, akiwa na dhambi zetu, akifa, akinena kwa lugha nyingine, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?"

67 108

Huo ndio Ujumbe wa Kanisa. "Katika Jina Langu mtatoa mapepo; watanena kwa lugha mpya." Hilo ndilo Yeye alilosema. Huo ndio Ujumbe wa Kanisa. Hilo ndilo Yeye aliloamuru Kanisa lifanye, "Kutoa mapepo; watanena kwa lugha mpya."

Watashika nyoka; hata wakinywa kitu chenye madhara hakitawadhuru kabisa; wata ... weka mikono yao juu ya wagonjwa, ... nao watapona.

Hilo ni agizo kwa Kanisa. Hilo ni kanisa halisi, linaloamini.

Je, hilo linafundishwa katika Methodisti, Baptisti, Presibiteri, Katoliki, Lutherani, Nazareti, Pilgrim Holiness? [Kusanyiko linasema, "Hapana."-Mh.] Hapana, bwana. Wao hulikana Hilo. Utukufu! Kwa nini? Wao wameundwa kuwa shirika la dini, nao hawawezi kufanya hilo. Kuna washirika wengi ndani mle wanaoliamini Hilo, lakini hawawezi kusema lolote kuhusu Hilo, kwa sababu watatengwa na ushirika. Hiyo ni roho ya mpinga-Kristo, iliyofanya wawe shirika la dini.

Kanisa la Mungu aliye hai limezaliwa likiwa huru kwa Roho wa Mungu, halihitaji dhehebu lolote. Wao humfuata Mfalme wa Ufalme wa Kimasihi. Hawahitaji kuchukua msemo wa watu. Wao wamezaliwa wakiwa huru, waliwekwa huru na Mwana Ambaye huwafanya wao huru kweli kweli. Ishara hizi zitafuatana nao.

68 110

Hii Injili itahubiriwa. Ni nani anayekwenda kuihubiri? Mungu anaweza kuwachukua wasio na elimu. Mungu anaweza kuinua mawe, wawe watoto kwa ajili ya Abrahamu. Mungu anaweza kufanya chochote Yeye anachotaka kufanya. Yeye ni Mungu, na hivyo ndivyo Yeye hufanya. Yeye alipokuja, kamwe hakumwita Kayafa. Kamwe hakumwita kuhani yeyote. Kamwe hakumwita mwanathilojia hata mmoja. Yeye aliwachukua wavuvi, wachungaji wa kondoo, na wajinga na watu wasio na elimu. Biblia ilisema kwamba, "Petro na Yohana walikuwa yote mawili wajinga na wasio na elimu." Lakini Yeye aliweza kuwapa wao, na kutenda kazi kupitia wao, Ufalme wa Mungu, na kushangaza macho na akili za wenye hekima na wenye nguvu. Wao walisema, "Waliwaona wao kwamba walikuwa watu wajinga na watu wasio na elimu, lakini walizingatia jambo moja juu yao, kwamba walikwishakuwa na Yesu." Kwa nini? Walikuwa na Roho Wake juu yao. Wao walikuwa wanatenda kama Yeye alivyotenda. Wao walikuwa wanafanya mambo ambayo Yeye alifanya. Hilo ndilo hasa Yeye alilosema lingetukia. Ufalme wa Kimasihi. Ee, ninafuraha iliyoje juu ya haya mambo. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hakika. Ishara zitawafuata wao.

69 Sasa, jambo lingine ambalo hili Kanisa litafundisha, litakuwa uponyaji wa Kiungu, Ujumbe wa Kanisa. Nililinukuu tu hilo. Mathayo 10, Yeye alipolituma Kanisa Lake huko na huko. Hebu twende tu kwenye Mathayo 10:1, na tuone, kwa dakika moja. Tazama kile Yesu alichosema alipoliweka wakfu Kanisa Lake na kulitumikisha.

Na ndipo yeye ... akawaita wanafunzi wake kumi na wawili, akawapa mamlaka dhidi ya pepo wachafu, kuwatoa nje, wawatoe hao nje, na kuponya kila namna ya maradhi, na kila namna ya wagonjwa. (Agizo la kwanza kwa Kanisa Lake.)

70 112

Agizo la mwisho, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkahubiri Injili. Yeye aaminiye, anabatizwa." Hebu nilinukuu Hilo jinsi lingepasa, jinsi Hilo lilivyowekwa. "Enendeni ulimwenguni mwote, na kwa kila taifa, na kuonyesha nguvu za Roho Mtakatifu. Yeye aaminiye juu ya Hili na kubatizwa ataokoka. Yeye atakayelikana Hilo, atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapona; watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya. Hizi zitakuwa ishara zitakazofuata." Ile aya ya mwisho inasema:

Na wao wakarejea ... Bwana akitenda kazi pamoja nao, akilithibitisha Neno Lake kwa ishara zilizowafuata.

71 113

Hivyo ndivyo lilivyokuwa Kanisa la kwanza. Na, sikilizeni, Yesu alisema, "Mimi ni Mzabibu, nanyi ni matawi." Na kama tawi likileta mzabibu, na ule mzabibu ukazaa zabibu, tawi lingine litakalofuata, litazaa kama tu hilo tawi la kwanza lilivyofanya.

114

Ee, unasema, "Ndugu Branham, lakini, vema, tazama haya makanisa." Hiyo ni mizabibu iliyopandikizwa.

Sasa, unaweza kupandikiza tunda mojawapo ya machungwa au malimao na mi. Unaweza kuchukua mchungwa na kuweka limao juu yake na litaota. Hilo ndilo ninyi watu mlilopandikiza ndani. Na haya mashirika ya dini ndicho kitu mwanadamu alichopandikiza ndani. Ni limao, wakati wote. Litaota kwa sababu limeunganishwa katika jina la kanisa. Lakini, hebu niwaambie, kama huo mti utakujatoa tawi lingine, wenyewe, utazaa chungwa.

Na kama nguvu za Mungu zitazaa Kanisa lingine, litakuwa pentekoste nyingine. Na kitabu kingine cha matendo kitaandikwa nyuma ya Hilo kanisa, hilo ni sahihi, kwa sababu Hilo ni Kanisa la Mungu.

72 115

Yesu alisema, "Mimi ni Mzabibu. Ninyi ni matawi. Hamwezi kuzaa tunda mwenyewe,

lakini najitupa Mimi Mwenyewe ndani ya tawi." Na hilo lilizaa aina gani ya tunda? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

Kanisa la pili linainuka, Mwili wa siri wa Kristo utakuwa na ishara zile zile. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Bado ninyi mtaniona Mimi, kwani nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, katika kila tawi, hadi mwisho wa ulimwengu," Yesu Kristo yule jana, leo na hata milele. Hilo ndilo Kanisa la Mungu aliye hai. Hicho ndicho Yeye alicho. Hao ndiyo aina ya mashahidi Yeye alio nao.

73 Sasa, pia, Ni lazima Kanisa lifundishe ubatizo. Ni lazima hilo libatizwe. Hilo ndilo agizo. Yesu alisema hapa, katika Marko 16. Tutalitumia tu hilo. "Yeye aaminiye na akabatizwa." Amini, kwanza, na ndipo ubatizwe kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako, nawe utapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

118

"Na Roho Mtakatifu atakuja juu yako pia," atakuwa fundisho la Kanisa. Kwani, Yesu alisema, katika Luka 24:49. Tuko karibu kabisa na hilo, hivyo hebu tulifungue hilo, kwa sekunde moja tu, ile aya ya 49 hapa. Tulisoma ile ya 46 na 47. Itazame ile ya 49.

Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu: lakini ngojeni, au subirini (ngoja humaanisha "subiri") huku mjini Yerusalemu, hata mvikwe uwezo utokao juu.

119

Kama Kristo hakuweza kuruhusu kundi la wanaume, ambao walikuwa wametembea pamoja na Yeye kwa miaka mitatu na nusu, waende kuhubiri Injili yoyote, au wasingeweza kuhubiri Injili yoyote hadi wamsubiri Roho Mtakatifu,, Kanisa leo inapasa lifanye jambo hilo hilo. Limsubiri Roho Mtakatifu.

74 120

Nilikuwa ninaongea na bibi Mkatoliki, hapa siyo muda mrefu uliopita, katika Oregon, na yeye akasema, "Vema, unamaanisha kuniambia hilo kundi la wapumbavu chini kule ulikokuwa unahubiri, na wakipiga makelele na kulia, likiendelea namna hiyo, unamaanisha kwamba wao watakuwa Mbinguni, na kutawala Mbinguni?"

Nikasema, "Ndiyo, mama."

Akasema, "Vema, hatuamini katika vitu vya namna hiyo."

Nikasema, "Kwa sababu ninyi hamuamini Neno la Mungu."

Na yeye akasema, "Tunaamini kwamba Mariamu anatuombea sisi."

Nikasema, "Hilo ni la kipagani kabisa."

121

Yeye kamwe hakuwa mungu mke. Yeye ni mwanamke. "Mama wa Mungu," Mungu angewezaje kuwa na mama? "Salamu Mariamu, mama wa Mungu," Mungu angewezaje kuwa na mama? Yeye alimzaa Mwana wa Mungu, Kristo Yesu. Hakuna mwanamke aliye muumbaji. Yeye anabeba mbegu ya mwanamume. Mwanamume siyo muumbaji, Mungu huumba uzima. Ni marudio tu ya-ya mpangilio, ambao Mungu aliweka, ili kuleta watoto. Mariamu, siyo mama wa Mungu. Mungu hawezi kuwa na mama, kwa sababu Yeye hakuwa na mwanzo au mwisho wa siku Zake. Yeye ni wa Milele. Mariamu hawezi kuwa mama wa Mungu.

75 122

Nikasema, "Vipi kama nikikwambia kwamba bikira wenu mbarikiwa, huyo mnayemwona kama mungu mke, vipi kama nikikwambia kwamba Mungu hakumruhusu kuja Mbinguni hadi atende kama wale watu walivyofanya usiku uliopita?"

Akasema, "Hilo siyo sahihi."

123

Nikasema, "Je, uliniambia kanisa Katoliki liliandika Biblia, mitume, na ulisema wao walikuwa Wakatoliki? Nalikataa hilo. Hapakuweko na kanisa Katoliki kwa miaka mia tatu baada ya kifo cha mtume wa mwisho, hadi baada ya Baraza la Nikea. Onyesha ukurasa mmoja wa historia, chochote unachotaka kuonyesha; siyo katekismo yako, kwa sababu hiyo hailingani na historia. Kamwe hapakuweko ha kitu kama hiki." Lakini nikasema, "Mariamu ... Biblia ilisema kwamba Mariamu, mama wa Yesu, na wale wanawake

wengine, pamoja na wale mia moja na ishirini, wote iliwapasa kupanda hizo ngazi kwenda ghorofani, na kujazwa na Roho Mtakatifu hadi wakayumbayumba kama vile walikuwa walevi, wakinena kwa lugha na kutenda kama kundi la walevi. Hilo ndilo Biblia ililolisema." Nikaweka kidole changu kwenye ile aya. Nikasema, "Lisome Hilo."

Akasema, "Sitaki kulisoma Hilo. Sipaswi kulisoma Hilo."

76 124

Nikasema, "Wewe siyo mwaminifu. Hapa ndipo bikira Maria alipompokea Roho Mtakatifu, na kunena kwa lugha na kuyumbayumba kama mwanamke mlevi. Sasa, kama wewe utakwenda Mbinguni, huwezi kwenda pamoja na yeye, kwa sababu ilimpasa yeye ampokee Roho Mtakatifu. Na kama ilimpasa yeye kufanya hilo, akiwa mama wa Yesu Kristo, ni kiasi gani zaidi unachohitaji hilo!"

125

Akasema, "Kama ingelinipasa kwenda Mbinguni nikiwa na kitu chochote kama hicho, singelitaka kuwa Mbinguni."

126

Nikasema, "Huna haja ya kuwa na wasiwasi. Usidhani kwamba unakwenda, hata hivyo, namna hiyo, isipokuwa ubadilike. Usidhani kwamba una mengi ya kusumbukia." Huyo ndiye Roho wa Mungu hasa.

77 127

"Sasa, ninyi ni mashahidi Wangu baada ya Roho Mtakatifu kuja juu yenu." Sasa, hiki ni kitu gani sasa. Tunasema nini? Hicho ni kitu gani? Ni nani aliyekiweka hicho? Na Ujumbe Wake ni nini? Sasa, ili kuharakisha, ili kwenda mbele zaidi kidogo.

128

Jambo la nne. Tunafanyikaje washirika wa Hilo? "Unajiungaje na Hilo? Tanaona kile Hilo lilicho, sasa nini? Tunajiunga vipi na hili Kanisa? Hujiungi na Hilo. Huwezi kujiunga na Hilo. Hakuna njia ya kujiunga na Hilo. Nimekuwa na familia ya Branham, miaka hamsini na moja, na kamwe sikujiunga na hii familia. Nilizaliwa nikiwa Branham. Nawe unazaliwa, ukiwa mwana wa Mungu au binti wa Mungu.

78 129

Hebu tuchukue Yohana, sura ya 3, kwa kitambo kidogo tu, na tuone tu kile Mungu alichosema hapa kuhusu Hilo. Unaingiaje katika hili Kanisa? Mungu anakupa pendekezo gani? Yohana, sura ya 3, 1 hadi 8.

Basi palikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo, mkuu wa Wayahudi:

Huyo alimjia Yesu usiku, akamwambia, Rabi, twajua ... ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu: ... kwa maana hakuna mtu awezaye kuifanya miujiza hii uifanyayo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.

Yesu akajibu, akamwambia, ... amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, ...

... amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.

79 130

Unaingiaje ndani ya Hilo? Unazaliwa ndani Yake. Hebu tuendelee kulisoma hilo swali zaidi.

Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, wakati akiwa mzee? ...

Mnamwona hhuyo mtu, wa kimwili, mwalimu, mtu mkuu, kuhani, mzee, aliyesoma Biblia maisha yake yote.

... aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?

Sasa, je, huyo siyo kama baadhi ya hawa walimu wasomi mnaowasikia leo hii?

Yesu akajibu na kumwambia, ... amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji... (Tunaingiaje ndani ya Hilo?) ... kwa maji na kwa ... Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.

80 131

"Yeye asije akajiunga na Hilo"? Huwezi kujiunga katika Hilo. Inakupasa uzaliwe ndani ya Hilo. Siyo "njoo ujiunge." Njoo uzaliwe!

Kile kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kile kilichozaliwa kwa Roho ni roho.

Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kuzaliwa mara ya pili.

Upepo huvuma upendako, ... na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda: kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.

132

Unaona, hujiungi na Hilo. Ni kitu cha kimafumbo. Unazaliwa ndani ya Mwili wa siri wa Kristo. Hivyo ndivyo unaingia ndani ya Hilo.

81 Wakorintho wa Kwanza, sura ya 12. Hebu twende mbele zaidi kidogo. Tunayo tu mengine zaidi machache ya kuendelea. Nataka kujaribu kuliweka katika uwazi labda kama nitaweza. Kama tu mta ... Najua kuna joto, lakini hebu tuanzie hapa, kwa dakika moja tu. Wakorintho wa Kwanza, sura ya 12, aya ya 13.

"Kwa maana kwa kushikana mikono kumoja, kwa kiapo kimoja. Naapa kuamini katika kanisa kuu takatifu la Kirumi. Njoo, shika mikono yangu. Weka jina lako kwenye kitabu. Kwa njia ya barua moja, ulikuja kwa njia ya barua"? Huenda mkawa mmesoma hilo katika Kitabu cha kumbukumbu ya matukio ya Siku ya Kuzaliwa ya Mabibi Wazee, lakini hamlisomi hilo katika Biblia ya Mungu. Ndiyo, bwana. Naam.

Kwa maana katika Roho mmoja (tulijiunga, tuliandikishwa?) sisi sote tulibatizwa katika (shirika moja la dini?) mwili mmoja, ambao ni Mwili wa Kristo, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Mataifa; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tumefanyika ... sote tulinyweshwa Roho mmoja.

Siyo roho ya Methodisti, roho ya Baptisti, roho ya Pentekoste. Bali, "Kwa Roho Mtakatifu mmoja sote tumebatizwa katika hii Chemchemi iliyojaa Damu."

Iliyovutwa kutoka kwenye mishipa ya Imanuel, Ambapo wenye dhambi walijitosa chini ya gharika, Doa lao lote la dhambi likaondoka.

Mwizi aliyekuwa anakufa alishangilia kuona

Ile Chemchemi katika siku yake; Pale na mimi niweze, japo ni mwovu kama yeye, Dhambi zangu zote zioshwe.

82 134

Mwili mmoja! Tunakujaje ndani ya huo Mwili? Tunaingiaje ndani ya Huo? "Kwa Roho mmoja tunabatizwa katika Mwili mmoja." Na tunapokuwa ndani ya huo Mwili, tuko huru, tuna hakikisho la ufufuo, "Mungu aliweka juu Yake maovu yetu sote." Siyo kwa "kushikana mkono kumoja," siyo "barua moja ya kanisa." Bali, "Kwa Roho Mtakatifu mmoja; Myahudi, Mataifa, wa njano, mweusi, wote wamebatizwa kwa Roho mmoja ndani ya huo Mwili, kupitia Damu ya agano Lake Mwenyewe." Na nionapo Damu, nitapita juu yako," na uko huru mbali na mauti, uko huru mbali na maumivu, uko huru mbali na dhambi. "Yeye aliyezaliwa na Mungu, hatendi dhambi, kwa sababu Mbegu ya Mungu hubakia ndani yake na yeye hawezi kutenda dhambi. Hakuna dhambi.

Yesu alisema, "Iweni wakamilifu, kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu." Unawezaje kuwa mkamilifu? Huwezi kufanya hilo. Wewe ulizaliwa katika dhambi, ukachukuliwa mimba hatiani, ukaja ulimwenguni ukisema uwongo. Lakini unapompokea Kristo kama mbebaji wa dhambi zako, unapompokea Yeye kwa imani, unaamini kwamba Yeye alikuokoa, na Yeye alikufa mahali pako na kuchukua dhambi zako, basi Mungu hukupokea wewe na kukubatiza katika huo Mwili na hawezi kuona dhambi tena. Nawezaje kuwa mwenye dhambi wakati kuna malipo ya fidia ya dhambi juu ya madhabahu kwa ajili yangu?

83 135

Polisi angenikamataje katika jiji, wakati amri za jiji zinanipa haki za kukimbia mwendo kasi wowote ninaotaka kukimbia? Huwezi kunikamata. Kama meya anasema, "Mchungaji Branham, unakwenda kuwahudumia wagonjwa. Nenda kwa kasi yoyote unayotaka kwenda, kwenye ukanda wowote," ananipa barua ya kuniruhusu hilo, hakuna polisi anayeweza kuniweka ndani. Kwa sababu meya ameniamini, kwamba singelifanya

hilo isipokuwa ilikuwa ni jambo la dharura.

136

Na Mungu aliponikubali na kunibatiza kwa Roho Mtakatifu, Yeye amekuwa na imani na mimi kwamba singelitenda dhambi kwa makusudi. Amina. Singetenda dhambi makusudi. Hivyo basi, Mwana Wake alilipa gharama ya ukombozi kwa ajili yangu, na mimi siwezi kuwa mwenye dhambi maadam nimehesabiwa haki na Yeye ameniweka ndani ya Mwili Wake. Nimekombolewa na Yeye. Siyo kile ninachotenda, bali kile Yeye alichotenda kwa ajili yangu. Hiyo ndiyo Injili.

84 137

Waefeso 4:30, "Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa Yeye mmefungiwa Kwake kwa lakiri hata siku ya Ukombozi."

138

Mhubiri mashuhuri wa Baptisti aliniambia, siyo muda mrefu uliopita, akasema, "Ndugu Branham, Abrahamu alimwamni Mungu, na kwa hilo hilo alihesabiwa haki. Yeye angefanya nini zaidi isipokuwa kumwamini Mungu?" Akasema, " "Tunaamini tunampokea Roho Mtakatifu tunapoamini."

139

Nikasema, "Lakini unakosea. Umekosea, japo u mwaminifu katika nia. Paulo alisema, katika Matendo 19, kwa wale Wabaptisti waliokuwa na mchungaji mzuri huko, mwanasheria aliyeongoka, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Yeye akasema, "Ile makala ya kwanza haisemi hivyo."

140

Nikasema, "Inasema hivyo. Ninayo makala ya Emphatic Doaglott. Na inasema hilo, katika kila fasiri, Kiyunani na Kiebrania. Yeye alisema, 'Je, mmekwishampokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?'" Nikasema, "Abrahamu aliamini, hilo lilikuwa kweli. Lakini Mungu alimpa yeye ishara kwamba Yeye alikuwa ameikubali imani yake, kwa kumpa yeye lakiri ya tohara." Hilo ni sahihi. Yeye alikuwa amemkubali yeye, kwa sababu Yeye alimpa Abrahamu ishara kwamba Yeye alikuwa amemkubali Abrahamu.

141

Kama unasema unaamini, na hujampokea Roho Mtakatifu bado, Mungu hajakufunga kwa lakiri bado, hajawa na imani ya kutosha kukuamini wewe bado. Unapokuja kwa Mungu, Mungu anakufunga kwa lakiri kwa Roho Mtakatifu hadi Siku ya Ukombozi wako. Na huo ndio Ujumbe wa Kanisa. Amina.

85 Tuendelee mbele zaidi kidogo. Vema. Sasa, Wakorintho wa Kwanza

12:13, "Kwa Roho mmoja tumebatizwa katika Mwili mmoja."

142

Matendo, hii hapa njia tunayoingilia hiyo. Huu hapa ufunguzi wa Kanisa, Matendo, sura ya 2. Wakati ujumbe wa kwanza ulipohubiriwa kwa Kanisa, baada ya Siku ya Pentekoste, wote walijazwa na Roho Mtakatifu. Maria, mitume wote, wote walijazwa na Roho Mtakatifu, wakinena kwa lugha, na wakipiga makelele tu kama kundi la watu walevi. Na walipokuwa tu na wakati wa kutisha, wakipiga tu kelele na kumsifu Mungu, na kuyumbayumba kwenye sauti ya ngongano ya Roho Mtakatifu. Wao hawakujali kama ilikuwa Jumapili, Jumatatu, ilikuwa ni siku gani. Wao walikuwa na wakati mkuu, wakipiga tu kelele na kuendelea mbele. Mbona, watu wakuu wenye akili walisema, "Hawa watu wamelewa kwa mvinyo mpya."

86 143

Sasa, hapa amesimama Petro akiwa na funguo wa Ufalme, pembeni mwake, funguo za kumfungulia Roho Mtakatifu. Yesu alisema, "Nasema wewe ndiwe Petro. Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayataushinda Huo." Ni kitu gani? Kweli ya kiroho iliyofunuliwa. "Nyama na damu havikukufunulia Hili. Hukuwahi kujifunza Hili katika seminari. Mtu fulani hakukufundisha Hilo, kutoka vitabuni. Lakini, Huo ni ufunuo unaona. Ufunuo! Nasema wewe ni Petro. Nakupa funguo za Ufalme. Lolote utakalolifunga duniani, nitalifunga Mbinguni. Lolote utakalolifungua duniani, nitalifungua Mbinguni." Ilipasa Yeye ashikilie Neno Lake. Kwenye Siku ya Pentekoste, ni

nani alikuwa msemaji? Petro, kwa sababu yeye alikuwa na funguo.

87 144

Na wao walikuwa wakimcheka, wakisema, "Hawa watu wameshiba mvinyo mpya.

145

Petro alisema, "Hii ikiwa ni saa tatu ya mchana, hawa hawakulewa mvinyo mpya. Lakini hili ndiyo Lile lililonenwa na nabii Yoeli, 'Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitamwagia Roho Yangu juu wote wenye mwili. Wana wenu na mabinti wenu watatabiri. Nitawamwagia Roho Yangu watumishi wangu wanaume na wanawake. Vijana wataona maono. Wazee wenu wataota ndoto, Na, naam, nitaonyesha ishara juu Mbinguni na nchi chini. Na itakuwa kwamba kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokolewa.'"

146

"Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, 'Wanaume na ndugu zetu, tutendeje ili tuokoke?'" Hili hapa agizo la Kanisa. Sasa wanataka kupata jinsi unavyoingia katika huu Mwili wa siri. Vema.

147

Matendo, sura ya 2, anzia kwenye aya ya 37, mahubiri ya uzinduzi. Huwezi kulibadilisha Hilo. Huwezi kulibadilisha Hilo. Sikiliza.

88 148

Kama daktari wako alikuandikia agizo la daktari la kupata dawa, na uipeleke chini kwenye duka la dawa, kwa mtoaji tapeli wa dawa, unajua, angeweza akukuua kwa kutumia lile agizo la daktari la kupata dawa. Unaona, huyo daktari anaandika kiasi hicho katika hiyo, kwa sababu yeye amefunzwa kwenye hilo. Na yeye anakuandikia kiasi fulani cha sumu, na yeye anaweka kiua sumu ndani pale ili kuua kiasi fulani cha sumu. Inampasa yeye aweke kitu fulani ili kupunguza nguvu ya ile dawa nyingine. Na kama zile dawa hazitatolewa sawasawa kabisa kulingana na vile tu daktari alivyoandika katika agizo lake, hiyo itakuua.

89 Na, hilo, Mungu ndiye Daktari. Yeye ni Daktari wa nafsi. Yeye ni Daktari wa wokovu. Na Yeye alimwelimisha mwanadamu katika Thiolojia Yake Mwenyewe, Petro, mtu asiyesoma ambaye hata asingeweza kusoma jina lake lilipoandikwa mbele yake. Lakini Yeye alimpa Roho Mtakatifu, na kumpa kalamu ya risasi ya kuandika juu ya Fundisho. Hivyo mnamo Siku ya Pentekoste, yeye aliandika Agizo la daktari. Hebu tuone kile yeye alichoandika. Daktari Simon Petro, hebu tuone Agizo lako la kidaktari kwa ajili ya ukombozi. Hebu tuone kile kilichaondikwa kwa ajili ya huo.

Walipoyasikia haya, wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na ... wale wengine ... mitume, Wanaume na ndugu zetu, tutendeje?

(Tazama, unazo funguo.) Ndipo Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja katika jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, ... kwa hao walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.

150

Hilo ndilo Agizo la Daktari. Usilibadilishe kwa kughushi; utamwua mgonjwa wako. Hilo ndilo tatizo la wengi wa hawa watu wanaozungumza hili, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Wanawaua watu wengi mno wa kiroho, wakiwapa kitu cha makosa.

90 Hakuna kitu kama hiki. Hakuna mtu aliyewahi kubatizwa, jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," katika Biblia. Hapajawahi kamwe kuwepo sherehe kama hii iliyowahi kutamkwa hadi kuibuka kwa kanisa Katoliki. Kanisa Katoliki ndilo mama wa hilo. Chunguzeni Maandiko. Chunguzeni historia na muone. Utekelezaji wa kwanza uliowahi kufanyika kwa "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," ulikuwa ni padre wa Katoliki.

151

Wao huwanyunyizia hao. Kunyunyizia maji kuliamriwa na kanisa Katoliki, "MAMA WA MAKAHABA." Tunarejea moja kwa moja chini kwa yule

"kahaba."

152

Inasemekana hivi katika katekismo, "Je, imewahi kamwe kutokea kitu kama Mprotestanti kuokoka?" Akasema, "Mara nyingine, bila shaka, kwa sababu wao hukubali fundisho la Katoliki." Wao hawazingatii Biblia yao. Wao hubatiza, jina la "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," na hawana Andiko kwa ajili ya hilo. Kasema, "Lakini kanisa Katoliki lilianzisha hili," na wao wanalikiri hilo. "Kwa Kwa njia ya hayo maagizo ya Katoliki, huenda wakawepo baadhi waliookoka." Hakuna kitu kama hiki. Hakuna mtu aliyewahi kubatizwa namna hiyo. Hakuna mtu aliyewahi kunyunyiziwa, katika Biblia, aliyemwagiwa, au njia nyingine yoyote.

Lakini, kuzamisha ndani ya maji, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Tumesoma nini kitambo kidogo kilichopita, na niliwaambia ninyi, tutalifikia Hilo baadaye? Kwamba, "Toba na ondoleo la dhambi lingehubiriwa katika Jina Lake." Hadi wapi? Hadi Yerusalemu tu, hadi kwa Wayahudi tu? "Kwa mataifa yote, ulimwenguni kote, kuanzia Yerusalemu."

91 Sasa, Daktari Simoni Petro aliandika hilo Agizo la daktari la kupata dawa.

154

Vipi kuhusu ninyi, madaktari, je, mnajaribu kuweka kitu fulani pamoja na Hilo? Msiongeze kitu chochote kwenye Hilo. Lichukueni jinsi lilivyo. Hilo ndilo agizo kwa Kanisa. Hivyo ndivyo unavyoingia ndani ya Hilo. "Kwa kutubu, na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu, na ahadi kwamba mtampokea Roho Mtakatifu." Sasa, hilo ndilo Biblia ililosema, "Kubatizwa kuingia katika Kanisa! Kubatizwa kuingia katika Kanisa!"

92 155

Hebu tusome Wagalatia 3:26, kwa dakika moja tu. Hatuna zaidi ya jambo moja, mawili zaidi, mambo matatu zaidi hapa, ndipo tuta-tutafunga. Sasa hebu tusome hapa katika Wagalatia, sura ya 3. Kama mtu yeyote ataipata kabla ya mimi, aisome hiyo. [Dada mmoja anaanza kusoma Wagalatia 3:26, "Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa watoto ..."Mh.] Endelea. ["Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu."] Wagalatia 3:26? ["Niliusoma huo."]

Huenda nimelisoma hilo kwa makosa hapa, basi. Huenda ikawa Wakolosai. Hebu tusome Wakolosai. Na-najua kule nilikokuwa ninaelekea. Hebu tuone kama ni Wakolosai 3:26. Hapana. Hakuna 3:26.

Hilo ni nini sasa, Wagalatia 3:26? [Huyo dada anasema, "Naam."-Mh.] Hapa, nimelipata hilo hapa. Hilo ni sahihi. Endelea kusoma, dada, Wagalatia 3:26, ukiwa ndiyo ulianza. Huu hapa, 26, 27 na 28. Sasa sikilizeni kwa makini. [Huyo dada anasoma Wagalatia 3:26-28, kama ifuatavyo.]

Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu.

Maana ninyi nyote mliobatizwa kuingia katika Kristo mmemvaa Kristo.

Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu.

93 156

Tunaingiaje ndani ya huu Mwili? Tunafanyaje hilo? "Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, kuingia ndani ya Mwili wa Kristo Yesu."

Sasa, kitu kingine kilicho Ujumbe kwa Kanisa ni, jinsi tunavyoingia katika Kanisa, kupitia utakaso. Na utakaso, Waebrania 13:12 na 13, "Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa Damu yake Mwenyewe, aliteswa nje ya lango."

158

Sasa, Waefeso, hebu twendeni hapa. Inatupasa tusome hilo moja. Waefeso 5:25, moja kwa moja kwa haraka sasa. Waefeso 5:25. Vema. Ndipo hapa, 5:25. Hapana, bado ninalo jambo la makosa. Hilo sikuliandika hapa kwa usahihi. Hebu tuone. "Kwa hiyo wahubiri na makasisi ..." Ee, ndiyo. Nilikuwa nikiandika hili, kwa haraka hasa, kitambo kidogo kilichopita, hivyo lazima nililichukua la makosa ... Ee, ninao ukurasa wa makosa. Ndiyo. Amina. Ndiyo. Vema.

94 159

Waebrania 12 na 13, "Kwa ajili hii Yesu naye, ili awatakase watu kwa Damu yake Mwenyewe, aliteswa nje ya lango."

160

Kwa hiyo, enyi watu, hivi ndivyo tunavyokuja na Kanisa: kwa kutubu; kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zetu; na ahadi kwamba tutapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, hakuna mhubiri anayeweza kututikisa tuingie katika Hilo. Hakuna kasisi ambaye anaweza kutuapiza sisi tuingie ndani ya Hilo. Lakini tunazaliwa kuwa ndani ya Hilo, na Mfalme wa Ufalme wa Kimasihi. Amina.

161

Sasa, hili tu, je, naweza kuleta hili moja zaidi? Hapa ndipo nilipokuwa napo. Ni wangapi watakaa na mimi kwa dakika chache tu zaidi? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Unaona? Ni ... Ni saa tatu na nusu, na wakati umepita.

95 162

Sasa, Je, tunaweza kufika Mbinguni bila Kanisa? Nitaleta tu maoni kadha juu ya hili, kwa sababu ninayo takriban dazeni moja niliyoandikwa chini hapa, kama mnavyoona. Lakini na-na ... jambo moja tu, ambalo inapasa tujue. Hapana, bwana. Huwezi kwenda Mbinguni bila kuwa mshirika wa hili Kanisa.

163

Sasa, jambo la kwanza,katika Yohana 3:5, Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho!" ("Tubuni, na mkabatizwe, kwa Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na ndipo mnazaliwa kwa Roho.") Kuzaliwa kwa maji, kuzaliwa kwa Roho! Isipokuwa mtu amepata Hili, hawezi hata kuingia Ufalme wa Mbinguni. Yeye wala hawezi kuuona Ufalme wa Mbinguni. Basi kama umezaliwa kwa maji na kwa Roho, wewe uko ndani ya Kanisa. Kama hujazaliwa kwa maji na kwa Roho, haupo ndani ya Kanisa, na huwezi kuuona Ufalme wa Mbinguni. Je hilo linaleta maana kwenu?

[Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Ni sahihi tu kabisa. Sasa, je, mlijua ...

96 164

Unasema, "Vema, Ndugu Branham, naamini," vema, sikiliza, "na sijawahi kumpokea Roho Mtakatifu." Hapana, bado huamini. Wewe unaamini tu kwenye imani yako mwenyewe. Unalo tumaini.

Kwani, katika Wakorintho wa Kwanza, sura ya 12, na aya ya 3. Hebu tulinyakue hilo tu kwa haraka tunapokuwa karibu na hilo kama mnataka. Wakorintho wa Kwanza 12, sura ya 12 na aya ya 3. Na tutapata hilo kwa haraka tu, na-na kusoma hili hapa, na tuone kile Bwana alicho nacho katika Hili kwa ajili yetu. Wakorintho wa Kwanza 12, na aya ya 3.

Kwa hiyo nawaarifu, ya kwamba hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu, kusema, Yesu amelaaniwa; wala ... hawezi mtu kusema ... Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu.

97 165

Hujui lolote kuhusu Hilo hadi umempokea Roho Mtakatifu. Unasema, "Nampokea Yesu Kristo kama Mwokozi wangu binafsi." Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu muamini? Kama sivyo, hata huwezi kumwita Yeye Bwana, kwa sababu Yeye siyo Bwana. Yeye ni Kiumbe cha kihistoria ambacho wewe, kwa imani, umekikubali. Lakini Yeye akiisha kuingia ndani yako, kwa njia ya Roho Mtakatifu, Yeye ni Bwana wako. Hakuna mtu awezaye kumwita, Yesu ni "Bwana," isipokuwa tu kwa njia ya Roho Mtakatifu; hadi mzaliwe kwa Roho wa Mungu, na Roho Mtakatifu awe ndani yenu. Ndipo, kama mko hivyo, mmezaliwa ndani ya huu Ufalme, na ninyi ni sehemu ya Kanisa. Ninyi ni Walioitwa, basi. Mnaliona hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Vema, sasa.

98 Je uzima unaweza kutoka kwenye mhindi isipokuwa huo mhindi uwe na uzima ndani yake? Kama mbegu ya mhindi inawekwa ardhini, moja inamea, na ile nyingine haimei. Ile isiyomea, je inaweza kuwa hai tena? [Kusanyiko linasema, "Hapana."-Mh.] Hapana kwa vyovyote vile. Hakuna kitu chochote ndani yake. Ingawa, ilivyo, itakuwa tu mbegu ya mhindi nzuri tu vile vile, inayofaa kwa kukaanga kama ile nyingine ilivyo.

Itatengenezwa tu mkate wa mahindi mzuri kama ile nyingine itakavyokuwa. Itaonekana nzuri tu kwenye rafu ya kuhifadhia kama ile nyingine itakavyoonekana. Lakini kama haina uzima ndani yake, haiwezi kuinuka tena.

167

Mtu ambaye ni mtu mwema, anaweza kuwa mshirika mwema wa kanisa kama anavyokuwa Mkristo. Mtu aliye mwema, anaweza tu kuwa raia mwema kama alivyo Mkristo; mtu mwema, mtu mwadilifu. Lakini yeye anapokufa, ndipo hapo, isipokuwa yeye awe amezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Kwa sababu, kila kitu kilichokuwa na mwanzo kina mwisho.

99 168

Mungu ndicho kitu pekee kilicho cha Milele na Milele. Kwa hiyo, sisi ni sehemu ya Mungu, kwa kupokea Uzima Wake. Yesu alisema, "Nawapa Uzima wa Milele na Milele." Neno la Kiyunani hapo ni Zoe, humaanisha "Uzima wa Mungu Mwenyewe." Na njia pekee utakayoweza kuishi tena ni kuwa na Uzima wa Milele na Milele, ambao ni Uzima Wake Mungu, kwa sababu uzima wako utapotea. Lakini Uzima Wake utainuka tena, kwa sababu Mungu ni wa Milelena Milele. Na ninyi mnao Uzima wa Milele na Milele, na mnaweza ... hamuwezi kufa kama ambavyo Mungu hawezi kufa. "Yeye aniaminiye Mimi anao Uzima wa Milele, na nitamfufua siku ya mwisho, nitamfufua tena." Uzima wa Milele ulio ndani yake utamfufua yeye.

100 169

Sasa, je, tunaweza kufika Mbinguni bila kuwa ndani ya Kanisa? Huwezi kuwa katika Kanisa hadi uzaliwe mara ya pili. Huwezi kwenda mbinguni hadi uzaliwe mara ya pili. Kama umezaliwa mara ya pili, wewe uko katika Kanisa. Hivyo huwezi kwenda Mbinguni hadi wewe ni mshirika wa hili Kanisa, na huwezi kuwa mshirika hadi uwe umezaliwa ndani Yake.

170

Na hebu niwakabe kidogo. Na huwezi kuwa mshirika isipokuwa Mungu amekuita kuwa mshirika. Sasa, unapaswa kuwa na furaha ilioje kwa hilo, kwani wewe ulichaguliwa tangu asili kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na jina lako ... Loo! "Majina yenu yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwanakondoo," Kitabu cha Kanisa, "kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu." Hiyo ndiyo Biblia.

Biblia ilisema, "Mpinga-Kristo," mashirika ya dini, kanisa Katoliki pamoja na hayo mashirika mengine, mashirika," yatawadanganya wote walio juu ya uso wa nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwanakondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu."

Yesu alisema,"Wale wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Hilo ni Neno Lake Mwenyewe. Siyo kile ulichofanya, bali kile Yeye alichofanya.

101 171

Hebu tuliweke hilo sawa, kwa dakika moja. Hebu tufungue Waefeso, sura ya 1, kwa haraka. Sikilizeni hili. Huyu ni Paulo. Sasa, ilimpasa yeye kuendelea mbele kwenye ukamilifu pamoja na hili Kanisa. Paulo analisema hili kwa Wakristo> Ni Wakristo wangapi walioko ndani hapa? Hebu tuone mkono wako. [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Vema. Hili siyo kwa ajili ya watoto, sasa. Hili ni-hili ni hao ambao wanaweza kula nyama. Sasa, sura ya 1, tazameni yeye analisema Hilo kwa nani.

Paulo mtume wa Yesu Kristo, kwa mapenzi ya Mungu, ... (siyo kwa kutumikishwa na askofu, siyo kwa shirika la dini).

... mtume (yeye aliyetumwa) kwa mapenzi ya Mungu, kwa watakatifu ( hao ni waliotakaswa, au walio watakatifu) walioko Efeso, na ... walio waaminifu katika Kristo Yesu.

172

Yeye analisema Hilo kwa akina nani? Kwa hao walio tayari katika Kanisa. Wewe unapokuwa ndani ya Kristo, uko ndani ya Mwili Wake. Je, hilo ni sahihi? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Basi ninyi ni washirika wa Kanisa.

102 Neema na iwe kwenu, na amani zitokazo kwa Mungu Baba yatu, na ... kwa Bwana Yesu Kristo.

Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni katika sehemu za kimbinguni ndani yake Kristo Yesu:

173

Yeye alifanyaje hilo? Alifanya hilo kwa kitu gani? Wao walikuwa wamefika Yordani. Walivuka kuingia Nchi ya ahadi, na walikuwa wamekaa katika sehemu za Kimbinguni katika Kristo Yesu. Hili hapa. “Aliyetubariki kwa pamoja kwa baraka za Kimbinguni,” fundisho la Neno, kama Kanisa, Walioitwa nje walio ndani ya Kristo Yesu. “Tunapokuwa tumekaa pamoja katika sehemu za Kimbinguni,” kama Kanisa, tunapozaliwa katika Kristo Yesu. “Watakatifu, Walioitwa nje,” loo, jamani, mtu fulani Yeye anayeweza kumfudisha jambo fulani. Yeye alikuwa na shida mno kwa Wakorintho, lakini siyo hili Kanisa. Yeye angeweza kuwafundisha, mambo makuu. Vema.

103 Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa ... ( Je, mnakumbuka Jumbe zangu mbili zilizopita?) baraka zote za rohoni katika sehenu za kimbinguni ndani yake Kristo Yesu:

Kama vile ...

Sikilizeni. Hebu hili liwashtue sasa.

Kama vile yeye alivyotuchagua (wakati uliopita) katika yeye ...

“Kwenye uamsho wa mwisho”? Je, nimelisoma hilo kwa usahihi? [Kusanyiko linasema, “Hapana.”-Mh.]

Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ... (Tazama hapa.) ... kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo.

Kwa kuwa alitangulia k-u-t-u-c-h-a-g-u-a ...

Tulifanya nini? Hakuna chochote. Kile Yeye alichofanya ndicho ninachokitazama. Yeye lifanya lini? Alituchagua, akaweka majina yetu kwenye Kitabu Chake, kwenye Kitabu Chake cha Kanisa, ili tuwe washiriki wa Mwili huu wa siri, kabla ulimwengu haujaanza.

Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu

Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake,

104 175

Loo! Inakupasa uwe katika hilo Kanisa, ndugu, kama utaweza, kwani Yeye anakuja kwa ajili ya Kanisa. Ni kanisa la namna gani? “Kanisa ambalo halina doa, au bila kunyanzi.” Tunawezaje kuwa hilo? Kwa kufa katika Kristo, kubatizwa kwa Roho Mtakatifu katika Mwili Wake wa siri, na upatanisho wa Damu ya Mwana wa Mungu ikiwa imekaa pale kwa ajili yetu kila saa ya siku. “Tumekutwa bila lawama,” hilo ni Kanisa, “lisilo na doa, au bila kunyanzi.” Yeye alituchagua ndani Yake, na kuweka majina yetu kwenye Kitabu Chake.

Biblia ilisema, kwamba, “Yesu Kristo alikuwa Mwanakondoo aliyechinjwa ...” Miaka elfu moja na mia tisa iliyopita? Umbali kiasi gani? “Mwanakondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

105 176

Wakati, “Mungu,” katika Biblia, lile neno katika Mwanzo, Mwanzo 1. Lilisema, “Hapo mwanzo Mungu ...” Chukua hilo jina Mungu katika Kiebrania, na uone linaaminisha nini. Linatamkwa El, Ela, Elohim, ikimaanisha “aliye yote, Yeye anayeishi Binafsi, anayejitosheleza, Yeye aliye mwenye uwezo.” Hapakuweko na kitu kabla ya Huyo. Hapakuwepo na hewa. Hapakuwepo na nyota. Hapakuwepo na unyevu. Hapakuwepo na-hapakuwepo na anga. Hapakuwepo na atomi. Hapakuwepo na molekuli. Hapakuwepo na chochote kabla ya Huyo. Ilikuwa ni Mungu, aliye wa Milele na Milele. Na ndani Yake kulikuweko na sifa, ili awe Mwokozi, awe Baba, awe Mungu. Huko, Yeye hakuwa Mungu, wakati huo. Yeye alikuwa-Yeye alikuwa Mungu, lakini hapakuwepo na chochote kingine, hakuna kuabudu. Hivyo, Mungu ni “kitu cha kuabudiwa,” na hapakuwepo na chochote cha kumwabudu Yeye. Hivyo kulikuweko na sifa ndani Yake ili awe hicho, awe Mwokozi, awe mponyaji, awe vitu vyote hivi Yeye alivyo.

106 177

Hivyo, jambo la kwanza Yeye aliumba. Sasa, baadhi yenu mnataka kujua kuhusu ile habari yangu ya Kitabu cha Mwanzo. Mungu alisema, "Na tufanye mtu." Kitu cha kwanza Yeye alichoumba kilikuwa Malaika, ili wamwabudu Yeye, ndipo Yeye akafanyika kuwa Mungu. Ndipo yeye aliposema, "Hebu na tufanye mtu kwa mfano Wetu," yeye aliumba mtu wa jinsi gani? Mtu wa roho. Ndipo, Yeye alipomfanya huyo mtu, Yeye alimpa udhibiti. Ndipo akafanya mtu kutoka mavumbi ya ardhi. Ndipo, yeye akaanguka; halafu Yeye akafanyika kuwa Mwokozi. Mungu, halafu Mwokozi. Dhambi ilileta magonjwa, ndipo Yeye akafanyika kuwa mponyaji. Haleluya! Hapakuwepo na chochote cha makosa. Yeye alijua yote kuhusu hilo, kabla ulimwengu haujaumbwa. Yeye alijua tungelikuwa na huu mkutano usiku huu. Yeye alijua kila kisubi ambacho kingelikwepo duniani, na angetoa ute kiasi gani, na ni mara ngapi angepepesa macho yake. Yeye ni Mungu asiye na mwisho. Yeye anajua mambo yote. Amina. Je, hamna furaha, usiku huu, kwamba jina lako liko kwenye Kitabu? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.]

107 Ni wazo jema lilioje ninalowazia

Juu ya Ndege mkuu mwenye madoa, Na wao husema kwamba Jina Lake limeandikwa Kwenye kurasa za Neno Takatifu la Mungu. Ndege wengine wote wakiruka kumzunguka, Hao wote wanamdharau Yeye.

178

Huyo ndege aliyekuwa na madoa ni yupi? Natofautiana na huyo mtu aliyesema Hilo lilikuwa kosa. Ndege mwenye madoa wa Biblia alikuwa yupi? Hakuwa Israeli, kama walivyosema. Ilikuwa ni Kanisa la Yesu Kristo.

Wao walifanya nini, kwa ajili ya dhabihu ya dhambi? Walimchukua njiwa, wakamkata kichwa mmoja na kumning'iniza, na kumwaga damu juu ya mwenziwe aliye hai, na kumwachia huru huyo mwenziwe aliye hai. Na huyo aliye hai, aliyenyunyiziwa, akiwa na damu ya mwenziwe aliyekufa, alikwenda kote duniani, akinyunyizia alipokuwa akipigapiga mabawa yake. Na damu ikitapakaa juu ya nchi, alilia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni kwa Bwana! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni kwa Bwana!"

108 179

Huyo alikuwa mfano wa Kristo. Na ndege mkuu mwenye madoa ni Kanisa lenye madoa kwa Damu ya Mwenzi Wake, Mwokozi, Yesu Kristo. Na Hilo linapita ulimwenguni leo, ukipigapipiga mabawa yake, likilia, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni kwa Bwana!" Amina! Nafurahi kwamba nalifahamu Hilo. Nafurahi mno jina langu liko kwenye Kitabu Chake, liliwekwa huko siyo kwa wema wangu; hapana, bwana, kamwe singekuwa Hapo, au kwa wema wako. Bali kwa wema na rehema za Mungu, kabla kuwekwa misingi kwa ulimwengu, aliweka majina yetu kwenye Kitabu Chake.

109 180

Kitambulisho cha Kanisa ni nini? Hilo linapaswa liweje? Hilo lilikuwa nini? Ni Kitu gani? Ni kundi lililoitwa.

Ni nani aliyeliweka Hilo? Yesu Kristo. Siyo askofu, siyo kanisa Katoliki, siyo Methodisti, siyo Luther, siyo Wesley. Hapana, bwana. Ni nani aliyeliweka Hilo? Yesu Kristo.

Ujumbe Wake ni upi? Toba, ubatizo wa maji, ubatizo wa Roho Mtakatifu, uponyaji wa Kiungu, wokovu.

Tunafanyikaje washirika wa Hilo? Kwa kuzaliwa upya ndani Yake.

Je, tunaweza kufika Mbinguni bila Hilo? Hapana, bwana. "Kwa maana hao waliokufa katika Kristo Mungu atawaleta pamoja na Yeye," na siyo-siyo mtu mwingine yeyote bali hao waliokufa katika Kristo. Yesu anakuja kwa ajili ya hao waliokufa katika Kristo. Waefeso 4, sura, alisema kwamba ... Hapana. Wagalatia, naamini ni hiyo, sura ya 4. Alisema, kwamba, "Hao waliokufa katika Kristo Mungu atawaleta pamoja na Yeye. Hao waliokufa katika Kristo Bwana atawaleta pamoja na Yeye."

110 181

Sasa, kwa hiyo, ni kundi lililoitwa, Mwili wa siri. Kristo aliuweka Huo katika utaratibu. Kabla Yeye hajafa, Yeye alinena juu ya kuja kwa Huo, alisema, "Nitakuja na kuwa Mfalme juu ya huu utawala. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona. Hamtahusika kwa lolote na ufalme wa ulimwengu."

182

Hiyo ndiyo sababu wao wako katika huku kuchanganyikiwa, kunakoitwa "Babeli." Mmoja, "Vema, Mungu abarikiwe, mimi ni Mpresibiteri. Mungu abarikiwe, mimi ni Mmethodisti. Mungu abarikiwe, mimi ni ..."

Mungu abarikiwe, mimi ni Mkristo. Amina. Hilo ndilo jambo lenyewe. Nitajuaje mimi ni Mkristo? "Ishara hizi hufuatana na mwamini." Unaona? Hiyo hapo kadi yako ya utambulisho. Siyo kusema, "Subiri kidogo, naamini ninayo kadi yangu ya ushirika." Hapana. Mimi sina yoyote. Ya kwangu iko juu Huko. Huenda nikapoteza hii hapa chini. Lakini Yeye aliniambia, "Kabla ulimwengu haujaanza," Yeye alinipa kadi yangu ya utambulisho, kwa kila mmoja ajaye katika Ufalme. Hiyo imehifadhiwa Mbinguni, hivyo kumbukumbu ziko wazi. Nina furaha. Ni ...

183

Mtu fulani alisema, "Nilimtafuta Mungu. Nilimtafuta Mungu." Hilo ni kinyume na Biblia. Ni Mungu anayekutafuta, siyo wewe unayemtafuta Mungu. Mungu alipanda na kushuka kwenye bustani ya Edeni, akiita, "Adamu, uko wapi?" Siyo Adamu akiita, Mungu, uko wapi?" Ilikuwa ni Mungu akiita, "Adamu, uko wapi?"

111 184

Ee, nina furaha mno kwamba mimi ni mshirika wa Huo mwili. Sivyo kwenu? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Ni na furaha mno juu ya hili Kanisa kuu. Samahani kwa kuwawacheleweshа mno. Lakini mnaamini katika hili Kanisa kuu? ["Amina."] Je, mnaamini katika Hilo? ["Amina."] Je, mnaamini Huo ni Mwili wa siri? ["Amina."]

185

Sasa, ninyi watu wa Katoliki, kitu pekee mnachopaswa kufanya kuwa mshirika wa Hilo ni kumpokea Yesu Kristo na kuzaliwa kwa Roho. Ninyi Baptisti, ninyi Methodisti, Presibiteri, Lutherani, chochote ulicho, sikilizeni hapa. Msifikiri ninachukuliana na Wapentekoste. Wao ni waasi walioasi kutoka Upentekoste asili kiasi hicho hicho walivyo hao wengine walio katika kanisa lingine lolote. Hilo ni sahihi kabisa. Wao waliingia katika hilo ili kupata jina na kujitangazia imani. Hivyo tu. Lakini, umiliki wa kitu chenyewe, hawana huo. Hilo ni sahihi. Kwa sababu, mnapozaliwa kwa Roho, mnafanyika kuwa kiumbe kipya, na Mungu anaanza kushughulika na ninyi wakati huo kama wana, na mnaongozwa kwa Roho wa Mungu. Haidhuru wewe ni wa shirika gani la dini, hilo halina ... Huo ni utaratibu mdogo wa kale wa kidunia, huo unakwenda kupita. Lakini je wewe ni mshirika wa huu Mwili mkuu wa siri wa Kristo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Kama siyo, hebu umpokee Yeye, usiku huu, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa kitambo kidogo kwa ajili ya maombi.

112 186

Tunapofikiria sasa, je kuna baadhi hapa wangeinua mikono yao na kusema, "Mungu, nakuinulia mkono wangu, nifanye kuwa mshirika wa hilo Kanisa, usiku huu. Nipe kule kuzaliwa, kwamba Hilo ni langu. Je, umeniita, Bwana? Basi nataka niwe mshirika wa hilo Kanisa. Mimi ni mshirika mmojawapo wa haya mashirika ya dini ya kidunia, lakini sijashiriki kimatendo. Sina nguvu kutoa pepo na kufanya haya mambo, kama Wewe ulivyosema yangefuatana na mwamini. Sijaipokea hiyo bado, Bwana. Na Wewe ulisema, "Ishara hiyo ita ... Ita humaanisha Wewe utafanya. Nipe nguvu, Bwana."

113 187

Mungu akubariki. Mungu akubariki, na wewe, na wewe, ninyi nyote mlioinua mikono yenu. Mungu awabariki na kuwapa hiyo nguvu, ili kuwa mshirika wa hili Kanisa kuu, Kanisa la Yesu Kristo.

Mtu mwingine, kabla hatujaomba? Mungu akubariki, bi mdogo. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki. Ndiyo, naona mikono yenu nyuma kule. Mungu akubariki, hapa, naona mkono wako, mwana. Naona mikono yako hapa, ndugu. Ndiyo. Mungu akubariki. Na wewe, mdogo kule, msichana mdogo. Mungu akubariki.

Mtu mwingine, inua tu mkono wako. Mungu akubariki huyu dada aliyeketi hapa. "Nataka kuwa mshirika. Nataka kuwa na Damu juu yangu, ninapotoka nje ya hili jengo usiku huu, kwamba niweze kutoka nje na maisha yangu yaseme, "Mtakatifu, kwa Bwana." Mungu akubariki wewe nyuma huko, mvulana. Mungu akujalie baraka. Mtu mwingine sasa, inua mkono wako? Mtu mwingine aseme, "Mungu, unirehemu."

Kama unatamani kuja hadi madhabahuni, kwa ajili ya neno la maombi, hali tunapoimba huu wimbo.

Njooni nyumbani, njooni nyumbani,

Ninyi mliochoka, njooni nyumbani

Kama huna uhakika kuhusu hali yako, nakualika uje.

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

*"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7*